

TUMEIONA NYOTA YAKE NA TUMEKUJA KUMSUJUDIA



Nayahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu kuwa hapa jioni ya leo, kwenye kusanyiko hili zuri la watu Wakristo, kuwa na fursa hii kuwazungumzia kumhusu mbarikiwa Bwana wetu Yesu, Yule ambaye sote tupo hapa kumwadhimisha, kumpa Yeye heshima.

² Ni vyema kuwa na Ndugu Tony na Ndugu Williams, ma—marais wawili, wa tawi hapa Tu—Tu—Tucson na pia huko Phoenix. Tulikuwa na ibada huko juu Jumamosi iliyopita asubuhi, hakika tulikuwa na wakati mzuri huko katika ile Hoteli ya Ramada huko juu. Na tunatarajia kuwa na wakati mwingine mzuri huko, kuanzia tarehe kumi na tisa mwezi huu, ambapo ni majaliwa yangu kurudi kwa ajili ya ibada ndefu. Tunazo, naamini, ni siku nne usiku, kuanzia tarehe kumi na tisa. Pia nadhani Mkutano wa Kimataifa wa Wafanyabiashara unaanza tarehe ishirini na mbili, ishirini na tatu. Niko huko hadi tarehe ishirini na mbili, halafu nina si—siku moja ama mbili usiku, nafikiri, kwenye—kwenye mkutano wao. Kwa hiyo, haya ni majaliwa makubwa kwangu mimi kuwa na fursa kukutanika pamoja na Wakristo katika sehemu mbalimbali za nchi, kueleza hisia yangu na upendo kwa Kristo, pamoja nao, na kuwa na ushirika mzuri pamoja. Na sasa nasikitika sikufika hapa kufurahia chakula hiki kizuri ambacho ninajua mnacho. Ila nafikiri. . .

³ Nimekuwa huku nje kwenye usaili, nikiwaombea wagonjwa, na kujaribu kumsaidia mtu safarini. Na huu ni maskini ulimwengu mgonjwa, ambao tunaishi ndani yake, magonjwa mengi sana na matatizo. Lakini katikati ya haya yote, si ni jambo la ajabu sana kwamba tunaye Mtu fulani ambaye tunaweza kumtazamia, juu ya mambo haya yote, tupenyeze kupita haya.

⁴ Vipi kama hakukuwa na Krismasi halisi? Kama hakungalikuwapo na Krismasi halisi, vema, mambo yasingalikuwa jinsi yalivyo usiku wa leo. Kama hakungalikuwapo Krismasi, hakungalikuwapo wokovu wowote. Na sasa kwa vile tunaikabili Krismasi, tena, ni mbaya sana kwamba tumeibadilisha, maana yake halisi, kuwa ni kuzaliwa kwa Yesu, mpaka ninii tu, vema, inaonekana kana kwamba Baba Krismasi amechukua mahali pa Kristo katika Krismasi, na hadithi fulani ya uongo ya Kriss Kringle akishuka kupitia kwenye dohani, amebeba gunia la wanasesere mgongoni mwake, anayetembelea ulimwengu wote katika usiku mmoja. Nami sijui

basi kama tukihiheshimu Hilo kwa kulisoma, basi tunamheshimu Yeye kwa kuamini kile tulichosoma.

¹⁰ Kwa hiyo sasa, kutoa heshima ya kwanza, huku tukisoma Neno Lake, hebu tusimame kwa miguu yetu wakati ninapoenda kusoma sehemu ya Maandiko. Tunasimama katika heshima ya kulisoma Neno Lake. Ninaenda kusoma pale ninapotaka kuzungumzia usiku wa leo, kwa dakika chache tu. Itakuwa ni kutoka Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, hadithi ya Krismasi. Katika mlango wa pili wa Mathayo Mtakatifu, tunasoma hili.

Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi. . . zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu,

Wakisema, Yuko wapi yeye. . . aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia.

Basi mfalme Herode aliposikia hayo, alifadhaika, na Yerusalemu pia pamoja naye.

Akakusanya wakuu wa makuhani wote na waandishi. . . watu pamoja, akatafuta habari kwao, Kristo azaliwa wapi?

Nao wakamwambia, Katika Bethlehemu ya Uyahudi; kwa maana ndivyo ilivyoandikwa na manabii,

Nawe Bethlehemu, katika nchi ya Yuda; Hu mdogo kamwe katika majumbe wa Yuda, kwa kuwa kwako atatoka Mtawala, atakayewachunga watu wangu Israeli.

Kisha Herode akawaita wale mamajusi faraghani, akapata kwao hakika ya muda tangu ilipoonekana ile nyota.

¹¹ Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja, huku tukizungumza na Mwandishi wa Neno hili.

¹² Mungu mwenyezi, tunakushukuru Wewe usiku wa leo kutoka kwenye vilindi hasa vya mioyo yetu kwa ajili ya upendo wa Kristo ambao umekwisha kumiminwa katika mioyo yetu, katika siku hizi za mwisho, na Roho Mtakatifu. Tunakushukuru Wewe kwa sababu ya kuwa na majaliwa ya kukusanyika pamoja na kukuabudu Wewe, na tukiwa na hakikisho hili lenye baraka, kwamba, siku moja Wewe unalijia Kanisa Lako. Tunakushukuru Wewe, kwa kuwa wabeba Nuru wa wakati huu, kuwa hapa tayari kulidhihirisha Neno lililoahidiwa kwa ajili ya wakati ambao tunaishi sasa, tukijua kwamba hapo mwanzo Wewe uliligawa Neno Lako. Ukijua mwisho tokea mwanzo, kila wakati, Wewe uliligawa Neno Lako kwa wakati huo. Kwa njia fulani, hatujui jinsi hilo lilivyotendeka, bali katika kila mmoja wa nyakati hizo, tunapoangalia nyuma kwenye Neno Lako, na tunaona kwamba kulikuwa na upako uliokuja katika wakati huo, ambao

ulitimiza Neno hilo. Basi katika siku tunazoishi sasa, kuna Neno lililotengwa, ahadi kwa ajili ya wakati huu. Tunaamini kwamba Roho Mtakatifu yupo hapa duniani sasa, akijaribu kutafuta mioyo, kudhihirisha na kutimiza, kwa kuthibitisha Neno ambalo sasa limetabiriwa kwa ajili ya siku hii na majira haya.

¹³ Tukiangalia nyuma, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, kulikuwako na Neno ambalo lilikuwa limetabiriwa tangu bustani ya Edeni, la Mwokozi ajaye, na kulikuwa na Mmoja aliyekuja na kutimiza kila Neno lililotabiriwa. Maisha Yake yalithibitisha Neno la Mungu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno. Utimilifu wa Mungu ulikaa ndani Yake. Yeye alikuwa ndiye—ndiye Jibu na Utimilifu wa yote waliyokuwa wamesema manabii. Na sasa usiku wa leo tupo hapa tunakaribia, tena, sherehe ya siku Yake ya kuzaliwa.

¹⁴ Pia, Bwana, tunasikitika sana kujua kwamba hata taifa letu limejifunganisha lenyewe katika namna fulani ya ha—hadithi ya uongo ya mtu fulani ambaye alipaswa kuwa ni hadithi fulani ya kubuni ya uongo. Lakini, Bwana, tunajua kwamba mwaminio wa kweli anajua kwamba hilo ni kosa, na linafanywa tu na adui, kuondoa mawazo ya watu kutoka kwa Mungu wa kweli aliye hai.

¹⁵ Mungu, tunaomba kwamba Uwepo Wake utakuwa pamoja nasi usiku wa leo tunapoingia katika hadithi ya Krismasi. Pia jalia, Bwana Yesu, kama kungekuwa na mfanyabiashara mwanamume au mwanamke hapa katika je—jengo usiku wa leo, ambaye hajamkubali Yeye kama Mwokozi wao, jalia huu uwe ndio usiku ambao moyo wao wenyewe utafanyika hori itakayokuwa kitanda cha mtoto, usiku wa leo, kama ilivyokuwa wakati ule, Yesu aliyekataliwa na kudharauliwa, Masihi wa Mungu. Jalia waondoke hapa, usiku wa leo, huku Nyota ya Asubuhi ikining'inia juu yao, ikiangaza njia yao mpaka waweze kuvuka Yordani siku moja kwa Nuru yake Huyu. Tujalie, Baba, kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake na kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

Mwaweza kuketi.

¹⁶ Kwa kawaida kwamba kidogo ninazungumza kirefu; sitajaribu kuhubiri usiku wa leo, kwa sababu nimepwelewa na sauti. Bali ningependa kutoa mchezo mdogo wa kuigiza wa hadithi hii ya Krismasi. Na hapana shaka, ila kwamba mtaisikia mara nyingi, na Andiko lili hili likisomwa, litakuja kwenye redio zenu, kuingia kwenye televisheni zenu, na—na makanisani mwenu, wachungaji wenu wema na watiifu wa nyinyi wafanyabiashara, na kadhalika, wata—watasikia hadithi ya Krismasi, na watasimulia hadithi ya Krismasi, hasa.

¹⁷ Na sasa ningependa kuiendea tofauti kidogo na vile nilivyofanya Jumamosi iliyopita kwenye Tawi la Phoenix la Wafanyabiashara, juu ya ni kwa nini Yesu alizaliwa Bethlehemu.

Na kusingekuwa na mahali popote pengine Yeye angaliweza kuzaliwa, mnaona, kwa sababu ilinena Jina Lake na kile alichokuwa Yeye. Pia tuliona kwamba kote kupitia Maandiko, kwamba Yeye, Bethlehemu, ni Nyumba ya Mkate wa Mungu, na Yeye alikuwa Mkate wa Uzima wa Mungu. Na hakukuwa na njia... Na inatupa kujua basi kwamba sisi, Wakristo wote waliozaliwa upya, tumezaliwa Bethlehemu. Kristo ndiye Bethlehemu ya Mungu, Nyumba Yake ya Mkate wa Uzima wa Milele.

¹⁸ Sasa, usiku wa leo, tunaenda kuiendea kwa njia tofauti. Ninaenda kuchukua somo langu usiku wa leo, Bwana akipenda, *Tumeiona Nyota Yake Na Tumekuja Kumsujudia*.

¹⁹ Hawa mamajusi. Tunalo wazo hapa kwamba, na tunaambiwa hapa na mafundisho yaliyotokea zamani, kwamba kulikuwa na mamajusi watatu, ingawa hatujui hilo kuwa kweli. Biblia haisemi kwamba walikuwa “watatu.” Hata hivyo, nimekuwa na majaliwa ya kuhudumu kule India, mahali kule walikotoka, nao husafiri watatu-watatu. Hiyo ni kusema, tungali tunawaona. Hivi tu si muda mrefu uliopita nilikuwa India. Na hapa unawaona kwa namna fulani wamechuchumaa mtaani huku ninii yao, mchana, huku wameegemezana vichwa kila mmoja, huku wamefunga vilemba vyao, wakiketi hapo kwa namna fulani wako katika ndoto ya mchana. Hawaketi chini kabisa, wanachuchumaa tu chini. Na hiyo ndiyo sababu, nafikiri, kwamba tunaamini kulikuwa na mamajusi watatu, kwa sababu wao husafiri watatu-watatu.

²⁰ Ndipo wao wakasema, “Tumeiona Nyota Yake Mashariki na tumekuja kumsujudia.” Kwa maneno mengine, “Tumeiona ishara Yake ya wakati huu,” waliokuwa wakiishi ndani yake. Ilitabiriwa hivyo.

²¹ Unaona, ninaamini ya kwamba Neno la Mungu ni la Milele, kwani, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili, akakaa katikati yetu.” Kwa hiyo Neno kamwe haliwezi kubadilishwa, ni la Milele. Ni Mungu Mwenyewe katika—katika hali ya maandishi, ni Biblia, Neno la Mungu.

²² Hana budi kulihukumu kanisa kwa kigezo fulani. Na Yeye hawezi kulihukumu kwa kigezo cha mfumo wowote ambao tumejiundia, kwa sababu kila mmoja wa mifumo yetu imeundwa na wanadamu. Nalo halina budi kuhukumiwa. Basi ikiwa—ikiwa ungetaka kutokubaliana na useme, “Hapana, ninaamini umekosea hapo, Ndugu Branham. Ninaamini *wetu*.” Ama jamaa huyo mwingine angesema, “Vema, *wetu* ndio.” Basi ni upi ulio sahihi, wakati kuna mifumo mbali mbali mia tisa na kitu ya hilo? Kwa hiyo Mungu asingaliweza kuhukumu kanisa kwa tofauti mia tisa na kitu mbali mbali katika mifumo.

²³ Lakini kutakuweko Mmoja. Alisema Yeye “angeuhukumu ulimwengu kwa Kristo, Yesu Kristo.” Naye Kristo ni Neno, hivyo basi tutastahimili hukumu kwa Neno la Mungu.

²⁴ Sasa, Mungu kamwe hafanyi jambo bila ya kuonyesha ishara kwanza. Yeye hana hatia ya kuwahi kufanya jambo lolote ila kwanza—kwanza kulionyesha kwa ishara Yake.

²⁵ Basi hawa mamajusi walisema, “Tumeiona Nyota Yake Mashariki,” walikuwa Mashariki wakati walipoiona Hiyo, ambayo ilikuwa huko Babiloni, iliyokuwa mashariki mwa Yerusalemu; nao walikuwa Magharibi, miaka miwili baadaye, wakisema, “na tumekuja kumsujudia Yeye.”

²⁶ Mapokeo ya Kikristo yanatufanya sisi kumjia mtoto mchanga, aliyelazwa katika hori, mamajusi. Hivyo sivyo ilivyo. Maandiko ni kinyume na hayo. Maandiko yanasema, “Walimjia mtoto mdogo,” si mtoto mchanga. Herode aliwaua watoto wote kuanzia miaka miwili kurudi chini. Unaona, pia angalia mahali palipowabidi kusafiri kwa ngamia kufika kule, iliwachukua moja kwa moja miaka miwili kuimaliza safari hiyo, wakiteremka, kupitia Mto Tigris na kuvuka. “Tumeiona Nyota Yake,” wakati walipokuwa Mashariki, “na tumekuja magharibi kumsujudia.”

²⁷ Sasa angalieni, Krismasi sasa imebadilika. Sasa, siku yenyewe ya Krismasi, sisi...hiyo ingebishaniwa, kwa sababu hatuijui. Jinsi tunavyoichukulia Krismasi, kama uliwahi kuichunguza, tunachukua dha—dhana ya kanisa la Katoliki ya Kirumi la wakati Krismasi ilipokuwa. Kwa kweli, Kristo asingaliweza kuzaliwa siku ya ishirini na tano ya Desemba, na iwe ni kulingana na Maandiko, kwa sababu kuna futi thelathini ya theluji katika Uyahudi wakati huo, unaona, kwa hiyo wao... isingewezekana wachungaji kuwa nje vilimani, na kadhalika, na ingekuwa kinyume basi na maumbile yote. Alikuwa kama maumbile.

²⁸ Kwa sababu, Mungu anayo kanuni, na kanuni hizo haziwezi kubadilishwa. Jua huteremka chini, huwezi kusema, “Vema, halitachomoza.” Huchomoza. Majira ya joto, vipindi vya baridi kali, na kadhalika, ni kanuni za Mungu ambazo Yeye ameweka katika utaratibu. Na hizo, kila moja, hufanya kazi kikamilifu.

²⁹ Sasa, lakini, Yeye labda alizaliwa Aprili au Mei, mojawapo. Wakati, Yeye alikuwa ni Mwana-kondoo, na kila kitu kingine kilithibitisha Yeye angekuwa ni Mwana-kondoo. Hiyo ndiyo sababu Yeye alizaliwa katika hori, kwenye banda, na si katika nyumba; kwa sababu wana-kondoo huzaliwa nje katika mabanda, kwenye majani makavu na kadhalika, na si katika nyumba. Wakati Yeye alipopelekwa kwenye kusulubishwa, aliongozwa. Kumbuka, wewe humwongoza kondoo. Tunaenda machinjoni hapa chini, wanaye mbuzi au kitu kingine kinachowaongoza kondoo; kondoo hataenda mwenyewe, hana

budi kuongozwa. Kwa kila njia, Yeye alikuwa, kwa hiyo basi katika maumbile ilibidi Yeye azaliwe wakati wana-kondoo wanapozaliwa. Na hiyo ni Aprili, unaona, huo ndio karibu wakati Yeye alipozaliwa.

³⁰ Lakini basi wakati Ukristo ulipoingizwa katika Urumi na kuchanganywa kule Nikea, basi walikuwa na mungu-jua, Jupiter, mungu-jua wa Rumi, siku yake ya kuzaliwa ilikuwa kwenye...kati ya...yapata siku ya ishirini na tano ya Desemba. Kwa sababu, sarakasi ya Rumi ilianza tarehe ishirini na moja na kuendelea mpaka tarehe ishirini na tano, ambayo ilikuwa katika kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa mungu-jua. Kwa hiyo kuingiza upagani wa Kirumi katika—katika Ukristo, walisema, “Hebu tuifanye siku ya kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu, ndipo basi tunaweza sote kukubaliana juu ya hiyo.” Unaona, daima imekuwa ni juu ya mifumo ya kupatana juu ya Kweli, kila wakati, daima imekuwa hivyo.

³¹ Kwa hiyo leo hii tunaona ya kwamba humo ndani wameingiza kila kitu, sikukuu zetu zote zimechafuliwa. Pasaka yetu, si tena ufufuo wa Kristo, ni namna fulani ya sungura wa Pasaka, ama kofia mpya, ama—ama kitu fulani, ama maskini bata mwenye rangi ya waridi; hazina uhusiano hata kidogo na ufufuo wa Kristo, si zaidi ya vile Baba Krismasi ana chochote kuhusiana na kuzaliwa kwa Yesu Kristo. Lakini ni ulimwengu! Nao ulimwengu wa biashara umeingiza kila kitu katika vurugu na mchafuko mpaka, si ajabu, Mungu ana haki kukitekeza kitu hicho. Na Yeye anaenda kukitekeza, Yeye aliahidi kwamba atakitekeza. Nao hauna budi kuingia katika mchafuko huu kusudi...Hakuna matumaini kwake, umekwisha.

³² Na sasa, bali katika majira ya giza hili, kama nisemavyo, ambalo tunaishi ndani yake, bado Wakristo wanapaswa kuwa wanaishikilia ile Nuru, kwamba kuna Kweli ya Krismasi, kwamba ni kuzaliwa kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Kimulimuli cha radi kilichopinda, na kilichogawanyika kwenye anga zenye hasira, zilizo na giza, na mawingu, zinaonyesha kunaweza kuwako na nuru kwenye giza. Inathibitisha kwamba kunaweza kuwa na nuru wakati wa giza.

³³ Hili ambalo ninazungumzia usiku wa leo, huenda likaonekana kidogo tu lisilo la kawaida, na hasa juu ya muhtasari huu na Maandiko niliyoandika hapa, ambao nitarejea, kwa vile wengi wao huandika Maandiko, na kadhalika. Sasa, kidogo si la kawaida. Lakini, ninawatakeni kila mara mkumbuke hili: Mungu si kawaida, Mungu hutenda mambo yasiyo ya kawaida. Hiyo ndiyo shida tuliyo nayo leo hii, tunagandamana sana katika mambo ya kawaida, hata, wakati jambo lisilo la kawaida linapotendeka, basi tu—tu—tuko nje ya hilo kabisa, hatujui ni kitu gani kimetendeka. Mungu huyafanya yasiyo kawaida. Na mtu yeyote aliyewahi kusoma Biblia, anajua kwamba Mungu daima hufanya yasiyo kawaida.

³⁴ Pia, kumbukeni, haya yote yamepangwa kimbele na Mungu Mwenyewe, kuzaliwa huku kwa Mwana Wake. Na wakati lilipaswa kutukia, na jinsi lilivyokuwa, na wakati lilipokuwa, yote yalipangwa kimbele na Mungu Mwenyewe.

³⁵ Je! mlitambua, ilibidi iwe tu katika wakati huu ambapo mfalme huyu mwuaji, Herode, si kitu ila mwuaji, aliwaua wale watoto wote, kusudi litimie lililonenwa na Bwana kupitia nabii, akisema, “Katika Rama, Raheli akivuna, akililia watoto wake, nao hawakuwako.” Mnaona, ilibidi kuweko na mfalme mwuaji kutimiza unabii ulionenwa mamia mengi ya miaka hapo kabla. Bali, wakati Mungu akilinenwa Neno kupitia nabii Wake, Hilo halina budi kutimia kama Hilo ni Neno la Mungu. Haijalishi kuwa Hilo linakawia muda mrefu namna gani, lingali litatimia kwa sababu Hilo ni Mbegu. Yesu alisema kwamba Neno la Mungu ni Mbegu ambayo Mpanzi alipanda. Kwa hiyo Hilo halina budi kuzaa matunda Yake katika majira Yake. Na sasa mfalme huyu mwuaji ilibidi awepo kwenye wakati huo, kuwaua hao watoto.

³⁶ Jambo jingine tunalotaka kuona ni, kwenye wakati huo wenyewe, kwamba ilibidi awatoze watu ushuru. Na, katika kufanya hivyo, hiyo ilimlazimisha Yusufu na mke wake (mke wake aliyemposa, Mariamu) kulazimika kurudi Bethlehemi.

³⁷ Mungu anajua jinsi ya kuyatenda mambo. Yeye atazifanya hata kazi za adui kumsifu Yeye. Wakati, tunawazia wakati mwingine kwamba yote “inatupasa kufanya *hili* na kufanya *lile*” ili kuifanya saa isonge sawasawa. Saa ya Mungu inasonga sawasawa, na Yesu atakuwa hapa kwa wakati unaofaa kabisa. Hatakuwa sekunde moja nyuma. Kila kitu kitatendeka vile hasa Mungu alivyosema kitatendeka. Kwa hiyo, kama tunafanya *hilo* ama kama hatulifanyi *hilo*, litakuwa hapa vivyo hivyo, maana Mungu amelinena, na litakuwa hivyo.

³⁸ Sasa tunaona, kwamba ushuru, ambao huyu Herode alisema kwamba watu wote waliokuwa wametoka mahali pao pa kuzaliwa, lazima warudi. Hiyo, alidhani alikuwa akitenda jambo kuu hapo, wakati alipofanya hili; na bila kujua kwamba alikuwa akifanya kazi katika upatanifu kabisa na Yehova. Ni makuhani wangapi ambao labda walimlaani Herode wakati huo, katika Jina la Bwana! Ni wangapi waliosimama, labda kisiri, na kusema, “Loo, huyu Mrumi, ninii... Kama tungaliweza kumkamata, tungefanya *hiki* na *hiki*, na *hiki*,” pasipo kujua ilikuwa inafanya kazi kulingana na mpango wa Mungu.

³⁹ Wakati mwingine, leo hii, tunaalani Ukomunisti na mambo haya yote. Ambao, nadhani, unafaa kulaaniwa. Lakini kama mngalijua tu ukweli, unafanya kazi hasa katika mkono wa Mungu, kufanya kile hasa Yeye alisema ungefanya. Hana budi kuinua kitu fulani kuondoa Babiloni kutoka duniani, na Yeye

anacho kifaa mikononi Mwake. Wewe yasome tu Maandiko, imeandika pale pale yale Yeye aliyosema angetenda.

⁴⁰ Na kama wale wahudumu wa siku ile wangelisoma tu na kuchunguza Neno hilo, wangelijua hilo ilibidi litendeke.

⁴¹ Sasa tunatambua kwamba juu ya kutozwa ushuru huu mkubwa, mfalme alitoa amri yake, ama agizo lake, kwamba watu wote wangerudi mahali walipozaliwa, haidhuru. Sasa, linaonekana kama jambo la karaha, maskini yule mwanamke mdogo, katika mahali pale alipokuwa, akiwa ni mja mzito, na ingebidi kufanya safari hiyo ndefu. Leo hii, ingekuwa vigumu kwetu kuwazia kumpeleka kwa gari la kuchukulia wagonjwa. Na ilimbidi kwenda. Kama uliwahi kuwa Palestina, na kuona mahali ilipombidi kupitia yale majabali ya matale, yanayoparua, kupitia huko juu, juu ya mgongo wa nyumbu mdogo. Haijalishi jinsi ilivyokuwa mbaya, na jinsi ilivyoonekana ya kikatili, hiyo ilikuwa ni amri ya mfalme, kila mtu sharti afanye hivyo, kijana au mzee, wamejiandaa au hawakujiandaa, iliwabidi kufanya hivyo, kwa vyovyote vile.

⁴² Pia wakati mwingine tunafikiria kwamba, mizigo yetu. Huenda nikaingiza hii papa hapa, kwamba, tunafikiria mizigo yetu ni mizito sana wakati mwingine, kwamba hakuna kitu kama huo ulimwenguni. Je! unajua kwamba mambo hayo yote ni mazuri kwako? Yote ni ya kukufinyanga wewe, kukuumba wewe. Manabii na wenye hekima walifinyanga upande wa nyuma ya jangwa, kwenye jua kali, linalowaka, kupitia dhiki na majaribu, na mateso. Na mambo haya tuliyo nayo leo hii, hakuna kitu kilichotendeka kwetu ambacho hakijawahi kuwatendekaa Wakristo wengine, hapo kabla. Wakristo wengine imewabidi kustahimili katika wakati wa giza kama huu, na hata kulishwa simba, kwa ajili ya ushuhuda wao.

⁴³ Halafu basi tunatulia, juu ya sifa fulani ndogo, ama mtu fulani tunaoidhania kuwa, “Vema! Vema, mimi ni mfuasi wa *Fulani na fulani*, kanisa hili fulani mlijualo. Ninahofia nitaleta aibu kama mimi. . .”

⁴⁴ Usihofie ushuhuda wako kwa ajili ya Yesu Kristo! Angaza Nuru yako! Simama imara kwa yale unayosadiki, kwamba “Yeye ni Mwana wa Mungu. Na huu si usiku wa kutembelewa na Kringle, Kriss Kringle, bali ni kuzaliwa kwa Yesu Kristo ndiko tunakosherehekea.” Mnaona? Sasa tunakuta mambo hayo kwamba yametendeka.

⁴⁵ Je! mliwahi kuwaona walipokuwa wanajiandaa kutengeneza kengele, kengele fulani maarufu kwa ajili ya kengele ya kanisa ama kitu fulani, iliyopaswa kutoa mlio fulani? Unaona, kama unapiga kengele, inahitaji mpangilio fulani kwa kila kengele. Na inahitaji madini fulani kuingia mle, kiasi fulani cha shaba, kiasi fulani cha chuma, na kiasi fulani cha madini mengine, kuingia katika kengele hii. Kama ni shaba tupu, haitalia sawasawa.

Lazima iwe na kila aina ya bidhaa itiwe mle, kuifanya itoe aina ya sauti ifaayo. Naye mtu aliyeiweka kalibu, na kuiandaa kalibu, anajua hasa kile kinachohitajika kuingia kwenye hiyo kuba, kinachohitajika kuingia katika hicho—hicho chuma, kuifanya kengele hiyo itoe sauti hiyo.

⁴⁶ Mungu ndiye kuba yetu kubwa. Mungu ndiye... Yeye ni Tanuru kuu la Mhunzi, mahali ambapo inambidi kuweka mambo haya juu yetu, na majaribu, na mateso na kadhalika, kuifinyanga pamoja, kuufanya ushuhuda wetu utoe sauti kwa muda fulani, na sauti fulani ambayo Yeye anataka isikike katika siku fulani.

⁴⁷ Tumeumbwa tofauti. Sisi sote tumeumbwa tofauti. Tunaona tofauti. Bali sote tunaona kitu kimoja, hicho ni Yesu Kristo. Hebu tumtazame Yeye. Na njia ya pekee uwezayo kumwona Yeye... Kama akionekana tofauti na Neno hili, humtazami Yeye, kwa kuwa Hilo ni Yeye. Kwa hiyo, kama unaona kanuni ya imani ama unaona dhehebu fulani ambalo unawazia tu, “Mimi ni mfuasi wa lile, na hilo latosha.” Kama haliangalii hilo Neno, basi ondoa macho yako kwalo. Litazame hilo Neno! Na hilo ndilo tunalotazamia, Kristo, dhihirisho la Neno la Mungu, Yeye ni thibitisho la Neno la Mungu.

⁴⁸ Sasa, mambo haya yote makuu, na yalitendeka huko chini kwa—kwa wawili hawa, linaonekana la kigeni. Lakini, linaweza kuonekana la kigeni kwao, bali lote lilikuwa linafanya kazi kwa wema.

⁴⁹ Sasa ndoto ya Yusufu, ningependa kuzungumzia hiyo kwa muda mfupi tu. Ninalo Andiko lililoandikwa hapa kwa ajili yake. Mungu, katika majira yote, nyakati zote, amewanenea watu Wake, na kujifunua Mwenyewe kupitia ndoto.

⁵⁰ Sasa, ndoto si hakikisho. Kila ndoto haitoki kwa Mungu. Sasa, wapo watu wengi ambao huwa na ndoto, na wanakuwa na kila aina ya ndoto. Nawe unaenda kulala usiku, na kula chakula kingi cha jioni na kwenda kulala, na huenda ukaota chochote. Unaweza kuwa na homa, na huenda ukawa na kila namna ya jinamizi, na kadhalika, hiyo si Mungu. Lakini, hata hivyo, Mungu hushughulika na watu kupitia ndoto.

⁵¹ Tunampata Yusufu mapema, mwana wa Yakobo, kwamba jinsi alivyokuwa nabii. Na nabii alielewa ndoto. Sasa, ndoto ikifasiriwa, basi inakuwa ono, ni unabii.

⁵² Sasa tunaona hata kabla ya hapo, mfalme Nebkadreza, na huko nyuma katika Danieli, na kote huko nyuma, kwamba Mungu alihusika na watu kupitia ndoto, ndoto za kiroho. Ninaziamini hizo. Tunazo sasa. Ni mara ngapi ningeweza kushuhudia, mamia ya watu ambao wamekuwa na ndoto, na kuzifasiri sawasawa, ilitendeka vivyo hakika!

⁵³ Lakini ndoto ni namna ya ki—kitu cha kubuni. Sasa, wakati mmoja chini ya uchunguzi, niliulizwa kuhusu ndoto. Na sasa ndoto ni wakati, tunaambiwa, uko kwenye dhamira

yako ya ndani. Sasa mtu anayo dhamira ya kwanza, na katika dhamira hii ya kwanza hisia zako tano zinafanya kazi, kuona, kuonja, kuhisi, kunusa, na kusikia. Lakini unapolala, ninii hizi tano... hisia hazifanyi kazi, ndipo basi uko hapa katika dhamira ya ndani, inayokaa mbali na wewe, ndipo basi uko hapo, unaota. Lakini unaporudi na kuamka... Bila shaka, ila kwamba hakuna mtu mmoja, si hata mtu mmoja hapa, ila ambaye umeota ndoto wakati mmoja maishani mwako, ambayo ungali unakumbuka. Basi kulikuwa na sehemu yako fulani, mahali fulani, ambapo uliporudi kwenye hisia zako tena, ungali unaikumbuka. Pengine ilikuwa miaka iliyopita. Ninakumbuka ndoto nilizoota nilipokuwa mvulana mdogo, ningali ninazikumbuka; basi inabidi kuwe na kitu, sehemu yangu fulani, ilikuwa mahali fulani. Sasa, hizo ni ndoto, kwa hiyo, unaona, uko mbali na hisia zako. Halafu wakati inaporudi na unasimulia ndoto yako, kama ni ya Mungu...

⁵⁴ Huenda kukawa na mfasiri wa ndoto. Biblia ilisema, “Akiwepo mmoja miongoni mwenu, aliye wa kiroho, nabii, Mimi Bwana nitajifunua Mwenyewe kwake katika ndoto, na kunena naye kupitia maono.”

⁵⁵ Sasa tunapata kwamba Yusufu, mwana wa Yakobo, alikuwa ni mtu wa namna hiyo. Kwamba, wangeota ndoto, halafu angeifasiri. Angeweza kufasiri ndoto, na aliona maono. Yote ni kazi ya Roho.

⁵⁶ Sasa tunapata pia, katika hili, kwamba mtu akizaliwa kuwa mwonaji, ama kuona maono, wewe—wewe ni... inabidi uitiwe hilo, na Mungu.

⁵⁷ Angalia, hii *hapa* dhamira yako ya ndani, ya kawaida, na hii *hapa* ni dhamira yako ya kwanza. Sasa inakubidi kuondoka kwenye hisia zako, hisia tano, uingie usingizini, ili kuingia kwenye dhamira yako ya ndani, ndipo urudi kwenye hiyo. Hiyo ni ndoto.

⁵⁸ Bali mwonaji, dhamira zote mbili ziko pamoja. Huondoki kwenye hisia hizi tano, ungali kwenye hisia tano, unasimama moja kwa moja na kuangalia kile kinachotendeka. Unaona, hutoki kwenye hisia zako. Uko pale pale, unajua mahali ulipo na kile unachofanya, ukiyanena maneno yako. Sasa, hiyo ni ka—karama iliyokusudiwa kimbele. “Karama na miito havina majuto.” Unaona, Mungu hufanya hayo. Huingii usingizini; unasimama huku macho yako yote mawili yakiwa wazi, ukiangalia moja kwa moja na kuona kile unachoangalia. Unaona? Na kile o—ono lililo, ni la Mungu, bila shaka.

⁵⁹ Tunalala leo hii. Hiyo ndiyo shida ya ulimwengu leo hii, unalala. Na watu wengi sana wanapenda tu kulala. Lakini mimi, nitasema hili, hakuna vitanda Mbinguni. Hatutalala tutakapofika Mbinguni, kwa kuwa hakuna usiku kule. Hakuna

usiku, kwa hiyo haitakubidi kulala utakapofika Mbinguni, maana hakuna vitanda kule.

⁶⁰ Lakini angalia, wakati dha—dhamira yetu, Mungu anaweza kutumia kila sehemu yetu ikiongolewa Kwake. Chochote tulicho, kikiwekwa kikamilifu mikononi mwa Mungu, na kuongolewa kwa ajili ya huduma Yake, Yeye anaweza kututumia katika ndoto, anaweza kututumia katika usemi, Yeye anaweza kututumia katika njia zote. Na yote tuliyo, yakigeuzwa kwa Mungu, basi Mungu anaweza kuyatumia. Je! mnaamini hilo? Mnaona, wakati tukiwa, kila kitu kimeongoka Kwake, Yeye anaweza kukitumia. Wakati utu wetu wote umeongoka, basi Wakristo wanaweza kuwa, siku hii, na ndoto za kiroho zinazoweza kumaanisha jambo fulani, zinazoweza kuwatabiria mambo. Tunajua kwamba hiyo ni kweli.

⁶¹ Ndoto ya kiroho inatafsiriwa, ikitafsiriwa sawasawa, ni sawa na ono. Nalo ono ni nini? Ono ni utabiri wa mambo yajayo; hueleza jambo kimbele kabla halijatukia. Na hivyo ndivyo Mungu daima alithibitisha kama lilikuwa ni kweli au si kweli, ama kama mtu huyo (hiyo ilikuwa ni katika Agano la Kale) alidhaniwa kuwa ni nabii, yale aliyosema yakija kutokea. Ndipo walijua; kama mtu huyu alisema hili, na daima liliendelea kutimia. Sasa, mtu huyo hawezi tu kuwa amewekewa mikono, ama kutikiswa, na kupewa ka—karama; anazaliwa na karama hiyo, inazaliwa ndani yake wakati anapozaliwa, kabla hajazaliwa.

⁶² Mwangalieni nabii Isaya, aliyetabiri kuhusu Yohana, miaka mia saba na kumi na mbili kabla hajazaliwa, akasema yeye alikuwa ni “sauti ya mtu aliaye nyikani.”

⁶³ Mwangalieni Yereimia, kabla hata hajachukuliwa mimba katika tumbo la mama yake, akiwa angali humo, Mungu alisema, “Nilikujua, na kukutakasa, na kukuchagua nabii kwa mataifa.” Mnaona? “Karama na miito havina majuto.”

⁶⁴ Na unaweza tu ukawa, hiyo inaweza tu kufanya kazi ikiwa kuna kitu humo ndani cha kufanya kazi nacho. Kama vile kama kuna mkono wa kulia kufanya kazi, nawe una mkono wa kulia, basi uache ufanye kazi kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Kama una macho ya kuona, basi vione vitu vifaavyo; midomo, sauti kunena, nena mambo yafaayo. Chochote kile, yafanye mambo yafaayo. Na uviongoe vyote ulivyo navyo, kwa Mungu, kwa utukufu Wake.

⁶⁵ Sasa, tunaona kwamba utabiri hueleza kimbele matukio yajayo kabla hayajatukia. La ajabu kama linavyoonekana, kwamba Mungu mwenyezi alitabiri, na kushughulikia masilahi ya Mtoto, Yesu, na kulifunua kwa ndoto, jambo la kufanya. Sasa vile Mungu, katika njia hii ya pili, kwa Mwana Wake Mwenyewe, alilifunua kwa Yusufu kupitia ndoto. Biblia ilisema Yeye alifanya hivyo. Naam, bwana. Sasa, Yusufu alikuwa ni mtu

mwema, alikuwa ni mwana wa Daudi, naye alikuwa amemposa Mariamu.

⁶⁶ Sasa ningetaka kuleta hili, kabla hatujaenda mbali. “Kuposa,” huko Mashariki, kulikuwa sawa na kuo, ni uchumba. Mara tu wao—walipoposana, walikuwa wameoana. Wakati nadhiri hiyo takatifu ilipofanyika kati yao, soma Kumbukumbu la Torati 22:23, na utaona kwamba wakati mwanamke huyu na mwanamume walipokubaliana kuoana (ingawa hawakuchukua nadhiri kwa miezi baadaye), ikiwa hata wangeivunja nadhiri hiyo, walikuwa na hatia ya uzinzi. Hiyo ni kweli. Walipoposana, walikuwa tu ni kama wameoana. Sheria haikuwa imewapatia haki ya kuishi pamoja kama mume na mke bado, lakini mbele za Mungu, walipoahidiana, maneno yao yalitiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu. Ndipo, kuvunja hiyo, kulikuwa tu ni kufanya uzinzi. Na sasa Yusufu alikuwa “amemposa” Mariamu. Ikiwa ndugu wahudumu, ikiwa mngechunguza hiyo vizuri, ingewaweka vizuri juu ya suala hili la ndoa na talaka ambalo ni gu—gumu sana na tofauti miongoni mwa watu leo. Sasa mwangalie Yusufu, mume wake, akiwa mtu mwenye haki, unaona, sasa tunaona kwamba hii isingeweza kuvunjwa.

⁶⁷ Akasema, hapana shaka alimwambia. Huyu mwanamwali mdogo, mrembo, msichana mdogo wa Kiyahudi, alikuwa... Sote tu watu wazima hapa, kadiri niwezavyo kuona. Alikuwa mja mzito. Naye Yusufu akitembea naye, alitambua jambo hili, bila shaka, baada ya kumposa, aligundua kwamba alikuwa mja mzito. Sasa, yeye alikuwa ni mtu mwenye haki, Biblia ilisema alikuwa. Hapana shaka alimwambia kuhusu kutokuwa na hatia kwake. Mwanamke huyo anayependeza, ninaweza kumsikia, kama tu vile kusema, “Yusufu, rafiki yangu mpendwa, mume wangu mpendwa, sina hatia katika jambo hili.” Na hapana shaka alimwambia kuhusu kuzuriwa, kwake na Malaika mkuu, kwamba Malaika mkuu alikuwa amemjia, Gabrieli, na alikuwa amemtembelea pamoja na ishara hizi kuu ambazo Yeye alikuwa amemwambia kuzihusu, kwamba kile kilichokuwa kinaenda kutukia.

⁶⁸ Halafu basi tunaona yeye, pia, baada ya kuwa na kuzuriwa huku, alifurahishwa sana na ujumbe wa Malaika, hata akaondoka kwenda katika nchi yenye vilima ya Uyahudi; kutoka Nazareti, ambako alikuwa ni mwenyeji, wa mji wa Nazareti, mji duni, mdogo sana.

⁶⁹ Basi alipofika huko juu, binamu yake Elisabeti alikuwa pia (tayari miezi sita) mja mzito, aliyekuwa ameitwa tasa.

⁷⁰ Mume wake, Zakaria, alikuwa kuhani hekaluni. Ndipo siku moja wakati alipokuwa akitikisa sadaka, ambao ulikuwa ni kufukiza uvumba, hasa, juu ya maombi ya watu yaliyokuwa yakifanywa huko nje. Gabrieli, Malaika wa Bwana; sasa, Yeye alikuwa hajaonekana, wala chochote kuonekana kuhusu

chochote cha Kimbinguni, kwa miaka na miaka, na mamia ya miaka. Bali hapa alisimama yule Malaika kwenye upande wa mkono wa kuume wa madhabahu, na kumwambia kwamba mke wake angechukua mimba na kumzaa mtoto, naye alikuwa anaenda kumwita jina lake “Yohana.” Na sisi sote tunaifahamu hadithi hiyo.

⁷¹ Ndipo basi wakati Gabrieli pia, miezi sita baadaye, alipomtembelea Mariamu huko Nazareti, na kumwambia kuhusu tukio la binamu yake, Elisabeti. Ndipo basi upesi, Mariamu akiwa na siri hii kuu moyoni mwake, kwamba kile kilichokuwa kinaenda kutukia, aliharakisha kwenda vilimani kwenda kumwona binamu yake.

⁷² Basi wakati Elisabeti alipokuwa amejificha, kwa sababu hakutaka kuonekana nje mbele ya watu katika hali aliyokuwemo, naye alikuwa amejificha miezi sita. Sasa, kulingana na ufahamu wangu wa Maandiko, alikuwa amefadhaika, mtoto hakuwa na uhai kufikia wakati huo. Na ilikuwa kabisa si kawaida kwa mtoto kutocheza tumboni, loo, angalau miezi mitatu, au minne, ya wakati. Bali sasa ilikuwa ni miezi sita, naye mtoto alikuwa hajasogea. Kwa hiyo wakati Elisabeti na Mariamu walipokutana, wao, hapana shaka, walikumbatiana, wakupigana pambaja, kama mabinamu, na—na walikuwa na furaha sana kuonana. Na hebu tuwazie tu kile walichosema. Ninaweza kumsikia Elisabeti akimwambia Mariamu, “Loo, kipenzi, unaonekana mrembo sana.”

Naye Mariamu akasema, “Unajua, ninajua kwamba una mimba.”

⁷³ “Naam, kwa namna fulani imenisumbua, na ni miezi sita na mtoto wangu hajasogea bado.”

⁷⁴ “Loo, lakini nina jambo la kukwambia, siwezi kabisa kulishikilia zaidi!”

⁷⁵ Unajua, lipo jambo fulani kuhusu wakati uapokutana na Mungu, huwezi kunyamaza kuhusu hilo. Inakubidi tu kusema jambo kulihusu, hiyo ni, kama ulipata wongofu halisi, wa kweli. Sijali mahali ulipo, huna budi kulieleza mahali fulani.

⁷⁶ Basi ninaweza kumsikia akisema, “Unajua, nina jambo la kukwambia. Mimi pia, ni mja mzito!”

⁷⁷ “Loo,” akasema Elisabeti, “Nadhani basi...Kwa nini hamkutualika kwenye arusi, wewe na Yusufu, wakati mlipofunga ndoa hatimaye? Ninajua mlikuwa mmeposana, lakini ni kwa nini hamkunialika kwenye arusi?”

“Loo, hatujafunga ndoa bado.”

“Na wewe ni mja mzito?”

“Ndiyo!”

“Vema, Mariamu, si—si—sielewi kabisa.”

⁷⁸ “Unajua, Malaika wa Bwana alinitokea, Gabrieli. Yeye alikuwa Ndiye aliyeniambia kwamba wewe ulikuwa ujifungue. Alikuwa Ndiye aliyeniambia. Pia Yeye alisema Roho Mtakatifu alikuwa anaenda kunitia uvuli; na Kitu hicho Kitakatifu nitakachokizaa, kitakuwa ni Mwana wa Mungu. Nami ‘nitaliita Jina Lake “YESU,” kwa kuwa Yeye atawaokoa watu Wake kutokana na dhambi zao.”

⁷⁹ Na mara ya kwanza ambapo Jina hilo la ajabu lilipotamkwa kwa midomo ya mwanadamu; maskini Yohana, akiwa amekufa katika tumbo la uzazi la mama yake, aliruka kwa furaha, na kupokea Roho Mtakatifu, akiwa amekufa katika tumbo la uzazi la mama yake. Kama—kama nguvu za kutajwa kwa Jina la Yesu Kristo zitamfufua mtoto aliyekuwa amekufa katika tumbo la uzazi la mama yake, zinafaa kulifanyia nini kanisa linalodai kuwa ni mtumishi Wake, lililozaliwa kwa Roho Wake? Kama vile Elisabeti alivyoshtuka, alipomwangalia Mariamu, alisema, “Imetokeaje mama wa Bwana wangu kuja, mama wa Bwana wangu? Maana mara sauti ya kuamkua kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto changu kichanga kikaruka ndani ya tumbo langu, kwa shangwe.” Yohana alizaliwa, kutoka tumboni mwa mama yake, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, kwa Jina la Yesu Kristo! Huyu anapaswa kuwa ni mtoto wa namna gani?

Hapana shaka kwamba aliyasimulia haya kwa Yusufu.

⁸⁰ Sasa unaona, Yusufu, akiwa ni mtu mwenye haki, kwa namna fulani alishangaa, “Unajua, sasa ninajua kama akipatikana katika uzinzi, kitu cha kwanza kinachoenda kumfanyikia, anaenda kupigwa mawe. Hawezi. . .”

⁸¹ Hawawezi kuishi namna hiyo. Biblia ilisema kwamba, “Pakiwa na kijana aliye mwanamwali ameposwa, akiwa mjini, na amebakwa na mwanamume, na asipopiga ukelele, basi wote wawili wapigwe mawe pamoja, wanauawa. Lakini akiwa mashambani, na kondeni, naye apige ukelele na pasiwe na mtu wa kumsikia, mwanamume huyo anafaa auawe, yeye mwanamwali ataishi.” Sasa basi, adhabu ya hiyo, hiyo ni Kumbukumbu la Torati 22, ambapo niliwautilizeni msome muda mfupi uliopita.

⁸² Sasa angalia sasa, katika hili, tunaona kwamba alikuwa mja mzito, hajaolewa. Kwa hiyo, kwa Yusufu, ilionekana kana kwamba Mariamu alikuwa akijaribu kumchukua kuwa kinga yake kutokana na wenye kukejeli na kudhihaki, unaona, Yusufu alikuwa awe ni ngao yake; apige hatua na kumwoa, kwa vyo vyote vile, na kuwa ngao yake, bali asiwe mume kwake katika u—uhusiano wa kifamilia, bali ilikuwa iwe. . . alikuwa awe ni ki—kinga kwa ajili yake.

⁸³ Alitaka kumwamini, na—naamini hilo kabisa. Alitaka kumwamini, lakini hadithi yake ilikuwa isiyo ya kawaida kabisa. Ilikuwa vigumu sana, kwa mwaminio huyo, kusadiki.

⁸⁴ Basi samahani, enyi wanaume. Na ndivyo ilivyo leo hii! Hadithi ya Nguvu za Roho Mtakatifu juu ya nchi leo hii, ndani ya Kanisa, si ya kawaida kwa nia ya shirika na ya kimadhehebu; mpaka hata wanataka kuamini Hilo, bali Hilo si la kawaida sana, Hilo ni la ajabu sana. Bali ni Kweli! Biblia ilisema ingekuwa namna hii, nalo Hili hapa. Watu wengi wamefungwa kwenye kanuni fulani ya imani, wanataka sana kuamini Hilo, bali Hilo si la kawaida sana hivi ni vigumu kabisa kwake kuamini. Ha—ha—hajui la kufanya. Yuko tu katika ha—hali ngumu kama alivyokuwa Yusufu.

⁸⁵ Biblia ilisema, “Alipokuwa angali anawazia mambo haya,” unaona, yeye alikuwa ni mtu mwema, na hakutaka jina lake mwenyewe lichafuliwe; na hata hivyo alijua, kama mwanamke huyo alikuwa namna hiyo, kwamba asingaliweza kumwoa, alikuwa ametiwa mimba na mwanamume mwingine. “Na hata hivyo,” alisema, “maskini mwanamke huyo, asiye na hatia, maisha yake yamekuwa safi kama yungiyungi, nami ninataka kumwamini, lakini si—sijui la kufanya.”

⁸⁶ “Alipokuwa akiwazia mambo haya, alitaka basi kumwacha kisiri. Akasema, ‘Sitasababisha usumbufu wowote mkubwa kuhusu jambo hilo.’” Sasa kumbukeni, alikuwa hajakula kiapo bado, lakini hata hivyo alikuwa amemposa. Bali angemwacha kisiri. “Basi wakati alipokuwa akiwazia mambo haya, ‘kumwacha kisiri,’ unaona, ilifikia upeo wa ufahamu wake. Unaona, alikuwa ni mtu mwenye haki, na mtu mwema.

⁸⁷ Ndugu, dada, hebu niseme hivi. Kama wewe ni mwenye haki, ukiwa mnyofu moyoni mwako, basi Mungu anawajibika kukufunulia jambo hilo.

⁸⁸ Yusufu, mumewe, akiwa ni mtu mwenye haki, alitafakari juu ya mambo hayo. Lilikuwa si kawaida kabisa, kama nilivyosema, i—ilikuwa vigumu kwake kuelewa hilo. “Mambo haya yangewezekanaje?” Lakini yeye, hapana shaka, aliketi chini, akaombea jambo hilo, akalichunguza katika Maandiko. “Mambo haya yangewezekanaje?” Huku akiwa anachunguza, Malaika wa Bwana alimtokea, katika ndoto. Hakuwa nabii. Pia hakukuwako na nabii nchini katika siku hizo, hakuna mtu angalimjia na BWANA ASEMA HIVI, kwa hiyo Bwana akachukua njia ya pili. Hiyo ndiyo sababu Mungu alichukua maslahi ya Mwana Wake Mwenyewe, kwa mwanadamu, katika ndoto; na kumweka Yeye huko Misri, na kumrudisha kutoka huko tena; na kumficha, kutoka kwa wenye hekima, ama watu wenye hekima walienda njia nyingine. Hakukuwako nabii nchini, kwa hiyo Yeye alichukua njia ya pili, ndoto. Lakini kulikuwa na watu ambao hawakuzaliwa kuwa waonaji, bali walikuwa ni watu wema, na, walipofanya hivyo, Mungu aliwazuru katika dhamira yao ya ndani, na akajifunua Mwenyewe.

⁸⁹ Kama utajisalimisha tu kwa Mungu, Mungu ana njia nyingi ambazo Yeye anaweza kujifunua Mwenyewe kwako. Unaona? Huenda isiwe, huenda usiwe nabii, huenda usiwe mwalimu, huenda usiwe mwalimu wa shule ya Jumapili, huenda usiwe mhubiri, bali kuna njia ambazo Mungu anaweza kujifunua Mwenyewe kwako, unaona. Hata kama labda ni ndoto, huenda ikawa katika njia nyingine, ikiwa tu utajisalimisha mwenyewe kama Yusufu alivyofanya.

⁹⁰ Hapana shaka alisema, “Ee Yehova Mkuu, Mungu, ni—nimekuja kupitia ukoo wa Daudi. Na mimi—mimi ni mtu mwenye haki; natumai ndivyo nilivyo, ninatumainia yale Wewe uliyosema kuwa ni Kweli. Naye maskini kipenzi changu, anayependeza hapa, niliye naye, nimemposa. Mimi, kumwacha kwa njia fulani, ni—nina hatia ya kufanya uzinzi. Na yeye ni mja mzito, nami simjui kama mke. Mambo haya ni nini, Bwana?”

⁹¹ Unaona, yeye hakuwa nabii, kwa hiyo Yeye asingeweza kunena naye kwa njia hiyo. Kwa hiyo Yeye—Yeye alimwacha aingie usingizini, na kumtuma Malaika wa Bwana kwake, katika ndoto. Amina. Malaika wa Bwana alimjia, katika ndoto, akamgusa, na kusema, “Yusufu, ewe mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu mkeo, kwa kuwa Hiyo mimba yake ni ya Roho Mtakatifu.” Haya basi, “Kilicho ndani yake, si mwanamume fulani, Roho Mtakatifu amefanya hili. Mwanamke huyo amesema kweli. Hadithi hii isiyo ya kawaida, jambo hili lisilo kawaida lililotendeka, Yusufu, ambalo limekufadhaisha mno, ni la Roho Mtakatifu.”

⁹² Loo, Mungu yeye yule angali anaishi usiku wa leo! Mngali mna dhamira ya ndani. Na nyinyi mna . . . Nyinyi Wakristo, ikiwa jambo hilo linaonekana lisilo la kawaida kweni, ambalo mnaona kwamba, ikiwa lingali sahihi hasa na Neno, basi Mungu anaweza kuyafunua mambo yasiyo ya kawaida katika njia nyingi.

⁹³ Kwa hiyo akamwambia Yusufu, “Ewe mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu wako, mkeo.” Kumbuka, tayari ni mke wake. “Jitwalie Mariamu, mke wako, kwa kuwa Hiyo mimba yake ni ya Roho Mtakatifu.”

⁹⁴ Sasa, ndipo Mungu akamtuma Malaika Wake, akaifunua, ufunuo Wake wa hiyo ndoto ikamjia Yusufu; alijua, hakukuwa na siri ndani yake. Malaika alimjia katika ndoto. Alimwona Malaika katika ndoto yake.

⁹⁵ Sasa, nabii, ama mwonaji, haingii usingizini, yeye humwona Malaika huku amesimama hapa. Mtu mwingine huingia usingizini, ndipo anaona Malaika.

⁹⁶ Naye Malaika akasema, “Sasa, Yusufu, hakuna kitendawili, hakuna mtu awezaye kukufasiria. Kwa hiyo, nitakueleza habari zake. Nitaifanya halisi kwako, maana hakuna mtu hapo anayeweza kuifanya halisi. Sasa usiogope kumchukua Mariamu, mkeo, kwa kuwa Hiyo mimba yake ni ya Roho Mtakatifu.”

⁹⁷ Ndipo wakati Yusufu alipoamka kutoka usingizini mwake, loo, jinsi moyo wake hapana shaka ulikuwa umejaa imani mpya iliyojaliwa. Lile fumbo lililokuwa limemsumbua, lile jambo fulani alilotaka kuamini, bali jambo lile alilojasiria kuamini, lilikuwa lisilo kawaida sana, hata hivyo lilijulishwa kwake kwa ndoto. Imani mpya ilichipuka katika maisha yake. Loo, jamani! Alikuwa na imani katika Mungu. Alikuwa na imani na mke wake, basi; zote mbili imani katika Mungu, na upendo kwa mke wake, na upendo katika yeye aliyempenda. Hakuna swali tena, hakuna swali tena kuhusu hilo. Alijua huyo alikuwa ni Malaika wa Bwana. Alijua kwamba Mungu alikuwa amemfunulia swali hasa lililokuwa niani mwake, kwa hiyo maswali yote yakaisha.

⁹⁸ Basi wakati Mungu, katika njia yoyote ambayo Yeye anataka kuifanya, anakufunulia swali lililoko niani mwako, hakuna shaka tena, hakuna swali tena kuhusu hilo. Ni ufunuo.

⁹⁹ Wakati unapoona jambo fulani hapa katika Maandiko, unasema, “Vema, sasa, ninaamini hilo lilikuwa tu kwa ajili ya mitume. Ninaamini Yesu alifanya hilo katika siku zilizopita.”

¹⁰⁰ Lakini Biblia ilisema, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele, ni Yesu yeye yule tu.” Basi ikiwa hilo linaonekana kuwa swali kwako, na unatafakari juu yake, huwezi kulelewa, nawe unaona jambo hilo linatukia, na unashangaa kulihusu; basi Malaika wa Bwana, kwa njia fulani, kama utakuwa mwaminifu, atakufunulia. Ndipo basi si swali tena, ni kweli basi. Loo! Ndipo basi unaweza kupiga mayowe na kupaza sauti, “Loo, ninashukuru sana!”

¹⁰¹ Ninaweza kuwazia vile Yusufu alivyohisi wakati jambo hilo lilipotokea, yote ilikuwa . . . siri yote ilikuwa imemalizika basi. Halafu, na wakati hili lilipofanyika, alionekana akishangilia, kwa sababu alikuwa na furaha. Sasa tunaona ya kwamba, moja kwa moja, alimwoa. Loo, hakuwa na swali tena. Alimchukua Mariamu, mke wake; naye hakumjua, kama mke, mpaka huyo Mtoto. Akafurahia jambo hilo! Alifurahia kuwa ngao yake Mariamu. Alfurahia kubeba shutuma yake.

¹⁰² Wakati mtu anapoweza kufunuliwa kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele; haijalishi ni kanuni ngapi za imani zinajaribu kuikanusha, una furaha kuwa ngao. Una furaha kuwa ngao. Wacha waseme chochote kile, unayo ngao kubwa huko juu kuondosha mishale ya moto.

¹⁰³ Ninatumai sitoi sauti kubwa kupita kiasi kwao walio huko nje. Hebu wasikie Hilo, pia, inawapasa kulisikia. Angalia. Naam, bwana.

¹⁰⁴ Una furaha kuwa ngao. Wewe ni mkeka wa mlangoni, chochote kitakachokuwa, haijalishi; imefunuliwa kwako na Bwana. Bwana amekuonyesha kwa Neno Lake, ni kweli; na kisha akakuthibitishia, kulifanya liishi tena. Unasema, “Hilo hapo! Jamani, hakuna kitu kinachoenda ku . . .”

105 Hakuna mtu aliye hata na haki ya kuhubiri Injili mpaka amekutana na Mungu uso kwa uso. Hiyo ni kweli. Hakuna mtu anayepaswa kuwa mimbarani bila ya kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Yesu aliwaagiza wanafunzi Wake, “Wasiendelee kuhubiri, bali wangoje katika mji wa Yerusalemu hadi mtakapovikwa Nguvu kutoka Juu.” Angalia kile Roho Mtakatifu alifanya wakati Yeye alipokuja. Naye Roho Mtakatifu ni Mungu.

106 Roho Mtakatifu ndiye Baba yake Yesu Kristo. Mathayo, mlango wa pili na kifungu cha 20, kinasema kwamba, “Mariamu, mama Yake, alipokuwa ameposwa na Yusufu, alipatikana na Mtoto wa Roho Mtakatifu.” Roho Mtakatifu ndiye Baba wa Yesu Kristo.

107 Basi Roho Mtakatifu ajapo na kufunua Neno, na kufanya Hilo liishi hasa, basi Hilo ni ufunuo kwako, unaona Hilo, limefunuliwa, Hilo limeahidiwa kwa ajili ya wakati.

108 Yusufu aliona hilo, kwamba huo ulikuwa ni unabii wa Isaya ukitimia. Isaya 9, “Kwetu sisi amezaliwa Mwana, tumepewa Mtoto. Ataitwa, ‘Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye nguvu, Baba wa Milele.’ Na Ufalme Wake hautakuwa na mwisho.” Alijua huyo angekuwa ni Nani, kwa sababu yeye—yeye aliona jambo hilo lote wakati Malaika wa Bwana alipomwambia hili, kwamba “Mimba aliyo nayo ni ya Roho Mtakatifu.” “Bikira atachukua mimba na atazaa Mwana.” Sasa, hiyo ilikuwa ni siri kubwa, ishara kuu ambayo Mungu aliupa ulimwengu wote, ishara kuu kwamba Huyu alikuwa ni Mwana Wake.

109 Sasa, angalieni tunapoendelea sasa. Sitachukua muda mrefu, nitajaribu nisichukue. Angalia tunapoona, ikiendelea, wakati Yesu... Sasa nafikiri ikiwa... Watoto wadogo hapa hawatatinii, hawataelewa, bali inanibidi kusema jambo fulani hapa kusudi watu wazima wataninii. . .

110 Wakati Kristo Yesu alipokuwa akiumbika ndani ya Mariamu, hapo ndipo mateso yalipoingia. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hapo ndipo mateso yake yalipoanza.

111 Na ni jambo lilo hilo ndani yenu. Wagalatia 1, ama Wagalatia 4:19, inasema kwamba, “Wakati Kristo (tumaini la Utukufu) alipoumbika, alipoumbika ndani yenu.” Kristo anaumbika ndani yako, wakati wewe unapokufa naye Kristo anakuwa Hai. Tazama mateso yakiingia, angalia shida zikianza kila mahali, mwangalie ibilisi akighadhibika, hakika, wakati Kristo anapoumbika ndani yako.

112 Basi wakati Kristo alipokuwa anaumbika ndani ya Mariamu, upesi ikaja amri ya mfalme, “Enyi watu wote!” Wakati alipokuwa tu akininii... Kristo alikuwa anafanyika Mtoto kamili, tayari kuzaliwa, papo hapo basi mateso makuu.

113 Sasa m—mtoto ameumbika kwa muda mrefu, moja kwa moja, katika tumbo la uzazi. Bali hii inakuja siku za mwisho, wakati ukamilifu, wakati utimilifu wa Uungu, wakati utimilifu

wa Kristo, unapaswa kudhihirishwa miongoni mwa watu Wake. Alisema hivyo, Yeye aliahidi hilo katika Neno Lake. Ndipo wakati utimilifu huo, unaona, yapo mambo yasiyo kawaida yanaanza kutokea, ambayo Yeye aliahidi. Hiyo ndiyo sababu maisha yetu mashuhuri ya kijamii na kadhalika hayawezi kuelewa hayo, Hilo ni upumbavu kwao. Sasa angalia, wanaunda Baraza la Mekanisa, unaona. Wakati tu Kanisa linapoanza kusimama kwa miguu Yake, ambapo nguvu za Kimbinguni zimeanza kufanya kazi, sasa wote wameingia katika kikundi, na sasa wanaenda kujaribu kukomesha jambo hili. Kama tu ilivyokuwa wakati ule.

¹¹⁴ Kama nilivyosema Jumamosi iliyopita, huko Phoenix, Wafilisti wamezunguka Bethlehemu, hata watu hawataweza kuja, isipokuwa waje kupitia Baraza hilo la Mekanisa. Loo, watawapeleka kwenye birika lililotuama; si kwenye maji safi ya Bethlehemu, bila shaka siyo. Sasa tunatambua.

¹¹⁵ Basi, wakati mfalme alipotoa amri yake, wakati tu Kristo alipokuwa anaumbika. Sasa hebu tuwachukue kwa dakika moja, hebu tuwatazame, tuwaendeleze tu kidogo kabla hatujafunga.

Ninaweza kumwona Yusufu akisema, “Mariamu, kipenzi, huyo mfalme katili!”

¹¹⁶ Lakini yeye angesema, “Sikiza, mpenzi. Kumbuka, Roho Mtakatifu aliniambia kwamba ‘Jina Lake litaitwa “YESU,” na Yeye atawaokoa watu Wake kutoka katika dhambi zao,’ watu Wake kutoka katika dhambi zao. Sasa, Yusufu, mpenzi, haijalishi kinachotendeka, na kile mfalme asemacho, mimi ninaweza. Ninaweza kuketi juu ya nyumbu mdogo. Ni maili kadhaa huko juu kuizunguka milima hii yenye mawe, na kadhalika. Na ikitokea kwamba tunahitaji usaidizi kidogo, kutakuwa na wengi safarini, maana sisi sio familia pekee. Wapo wengine waliopatwa na jambo lili hili lililotupata, kwa hiyo kuna wengine njiani. Na sisi kwa namna fulani tunaweza kuenda pamoja na umati wote wanapokwea kilima, na—na tupande kuingia Bethlehemu.” Kwa kuwa, kutoka Nazareti, wanapanda kuvuka mlima.

¹¹⁷ Sasa tunapata ya kwamba hapana shaka alimchukua maskini punda, na—na kumlisha fungu la ziada la nyasi kavu na shayiri siku hiyo, kwa sababu maskini mama huyo alikuwa mzito kwelikweli. Kwa hiyo anamketisha juu ya maskini nyumbu huyo, na kuweka mkoba wa maji na maskini biskuti chache; kisha anamchukua maskini punda, na kuchukua fimbo yake mkononi.

¹¹⁸ Basi moja kwa moja juu barabarani wanaanza, huko, maskini nyumbu anayumbayumba na kuanguka. Loo, angalia kile jamaa yule mdogo anachobeba! Angalia mzigo wake, kuwa ni nini! Anambeba Kristo kumpeleka mahali Pake pa kuzaliwa. Basi hapa, maskini mwanamke huyu anayeketi hapo juu, akiwa na utungu, kujifungua, huku ameshika manyoya ya

shingoni mwa maskini nyumbu huyo, na akizungumza naye huku akisafiri barabarani.

¹¹⁹ Ninaweza kuwaona, siku nzima, wangesimama na angempumzisha, na, “Mpenzi, hivi wewe—hivi umechoka sana?”

¹²⁰ “La, mpenzi, niko sawa. Niko sawa. Vema, hivi *wewe* ungetaka kupanda kidogo?”

“La, mpenzi, keti hapo.”

¹²¹ Basi angemtoa kwenye maskini punda, na kumpumzisha kidogo, kisha kumpa maji ya kunywa, na sandwichi ndogo. Kisha kumketisha tena juu ya nyumbu.

¹²² Hatimaye, giza likaanza kuingia. Wasafiri barabarani, wenye uwezo zaidi kusafiri haraka zaidi, nao wangukuja karibu. Basi ilimbidi kuvuta vumbi la hao wengine juu ya farasi na magari, na kadhalika, walioweza kupita. Kwa sababu, ilimbidi kusafiri pole pole sana, kwa sababu ya hali yake. Ni jambo katili jinsi gani kumpeleka mama huyo huko juu katika hali hiyo! Lakini ninaweza tu kuwazia sasa, katika mchezo mdogo wa kuigiza, wanapopanda kuja kwenye kilele cha kilima. Bethlehemu iko katika. . . kidogo kama bonde, na kwenye u—upande wa magharibi mwa mlima, wa—wa Bethlehemu, mlimani ambapo kinjia kidogo kinapitia.

¹²³ Ninaweza tu kuwaona sasa, katika mchezo wa kuigiza ninavyosema. Kunakuwa giza. Naye Yusufu anapigapiga kwa fimbo yake, njiani, huku akipitia kila njia ya mkato awezayo. Mahali njia ilipinda kuzunguka *huku*, ambapo ilibidi magari kuenda, vema, labda alipenya kupitia hapo kujaribu kuokoa wakati, kukwepa vumbi, pamoja na maskini mke wake. Nyota zikaanza kuonekana.

¹²⁴ Na, baada ya kitambo, anafika juu ya kilele cha kilima. Pia, ama, kwa mara nyingine wanaangalia kwenye mji walikozaliwa wote wawili, huko Bethlehemu, taa za mji. Wengi walikuwapo, sehemu zote zilijaa, watu nje, wakilala sakafuni, huko nje uwanjani. Ndipo swali, labda kwa mara ya kwanza, wakati huo likamjia Yusufu akilini. “Nitafanya nini ikiwa siwezi kupata mahali, maana Mtoto huyo huenda akazaliwa usiku huu. Amekuwa na utungu siku nzima. Kwa hiyo, sasa, vipi kama Mtoto huyo atazaliwa usiku huu?”

¹²⁵ Alipokuwa amesimama pale akiangalia chini kupitia kwenye bonde, akishangaa, ilitokea kwamba macho yake yaliangalia huko kando, ndipo akaona tamasha ya ajabu. Unajua, kwa kawaida huwa ni moja kwa moja wakati wa shida, ambapo mambo ya Kimbinguni hutokea. Aliangalia huko naye akaiona Nyota. Hakuwahi kukumbuka kuona moja kubwa hivyo. Ilionekana kuwa chini sana, na Hiyo ilikuwa imening’inia moja kwa moja juu ya Bethlehemu. Akaangalia juu, na akageuka, baada ya kumsaidia Mariamu kuketi juu ya jiwe kupumzika kidogo. Aligeuka ili kumwambia, “Mpenzi, hivi

ulipata kutambua..." Na yeye hata angeweza kuona uakisi wa Hiyo katika macho yake meusi, yanayopendeza, huku alipoketi na kutazama, akitabasamu. Kasema, "Mpenzi, Hiyo si ni ajabu?"

¹²⁶ Akasema, "Yusufu, mpenzi, nimeiangalia Hiyo tangu jua lilipotua. Nimekuwa nikiangalia hiyo Nyota. Kwa njia moja ama nyingine, ninajisikia visivyo kawaida kabisa usiku wa leo, kwamba jambo fulani linakaribia kutukia." Vema, kwa kawaida ni hivyo, mwajua, unakuwa na hisia hiyo ya ajabu.

¹²⁷ Ndipo akaanza kuiangalia hiyo Nyota, na Yusufu; yule, maskini nyumbu akipumzika, akihema. Nao wakaiangalia hiyo Nyota. Ilikuwa na tendo la kipekee Kwake. Haikutenda kama nyota zingine. Ilionekana kutotulia, ikisonga. Ilikuwa ikingojea kitu fulani, ikitazamia kitu fulani kutukia. Sasa hebu tuache maskini mume na mke wetu wameketi juu ya hili, juu ya hili jiwe, kwa dakika moja.

¹²⁸ Hebu tuweke niani mwetu na tuende, mbali mamia ya maili, huko mbali Mashariki, Mamajusi, huko juu Mashariki, huko India. Usiku huo, kama ilivyokuwa kawaida yao, wao wote, wakati nyota...jua lilipotua, nyota zilitokeza, walipanda juu mlimani, waliingia kwenye mnara, kwa namna fulani kama mnara wa uangalizi. Nao walipanda huko juu ku—kuabudu, na kusoma. Pia wao—wao walidumisha saa kwa nyota. Na walichunguza matukio, na—na wangepanda huko juu na wangepanda ku—kuanguka kwa mamlaka, na kwa mataifa, na kuporomoka kwa—kwa—kwa mataifa, na kadhalika, kwa falme. Na jinsi wangeweza, wangeweza kuwazia hayo na kuyazungumzia. Na walizijua hizo nyota, kila moja. Walizijua kama tunavyojua Biblia. Kila msogeo zilizofanya, ulimaanisha jambo fulani.

¹²⁹ Basi, mnajua Mungu daima hutangaza matendo Yake mbinguni kabla hajafanya hivyo duniani, hata hivyo. Wahudumu wanajua hilo.

¹³⁰ Hao hapo, wakizitazama nyota, kwa sababu wanajua kwamba mgeuko wowote, mara moja wanachunguza moja kwa moja kupitia kwenye Maandiko kuona kuwa ulikuwa ni kitu gani. "Unasema, 'Maandiko'?" Naam, Maandiko. Walikuwa Mamajusi. Lakini walikuwa ni Waislamu, kile ambacho kimekuja kuwa Uislamu. Walikuwa kwa kweli wametokana na Wamedi na Waajemi wa kale. Hapo ndipo Waislamu walipotokea. Sote tunajua hilo.

¹³¹ Pia, sikilizeni, walikuwa na kiongozi huko chini. Na kama unataka kulisoma, ni—ni Danieli 2:43. Danieli, nabii, alikuwa ni kiongozi wao wakati walipokuwa huko chini Babeli. Hiyo ni hakika. Danieli alikuwa kiongozi wao nabii. Naye alikuwa amewafunza mambo yote ya Mungu, maana alikuwa ni kiongozi wao. Basi aliwaambia ya kwamba, "kungekuwa na

Jiwe lililokatwa kutoka mlimani siku moja,” mnamkumbuka akilisema, “bila ya kazi ya mikono. Nalo lingeziponda falme za Kimataifa kwa ulimwengu, mnaona, falme zote, nalo lenyewe lingekua na kuifunika dunia.”

¹³² Na, sasa, hawa hawakuwa ni wasioamini, hawa Mamajusi. La, bwana. Walikuwa ni waaminio. Walimwamini Mungu mmoja wa kweli. Tunajua hiyo ni kweli, Biblia ilisema hivyo. Na kama unataka kulisoma, wewe soma katika Matendo 10:35, ambapo Hilo lilisema kwamba “Mungu hapendelei taifa lolote, bali anawaheshimu wale wanaomcha Yeye na kutenda haki.” Sasa, hata hivyo, hawakuwa hasa katika mkondo wa Kweli, bali walimwamini Mungu yeye yule tunayemwamini. Waislamu wanamwamini Mungu yule yule tunayemwamini.

¹³³ Nimesimama, mara nyingi, nikaona huyo kasisi wa Kiislamu akichukua kitu kile kikubwa pale, na kuugonga huu mshindo mkubwa pale, na kusema, “Yupo Mungu mmoja wa kweli aishiye, na Muhammed ni nabii Wake.” Tunaamini kwamba kuna Mungu mmoja wa kweli na aishiye, naye Yesu ni Mwana Wake. Unaona? Yeye anasema, “Na iwe mbali na Mungu kuwa na Mwana.” Anadhani ilibidi iwe ni roho, unaona, kwa hiyo a—akasema, “Yupo Mungu mmoja wa kweli na aishiye, na Muhammed ni nabii Wake.” Wangali wanamwamini huyo Mungu mmoja wa kweli. Ni watoto wa Ishmaeli.

¹³⁴ Sasa tunatambua kama walivyokuwa, kama hawa Waislamu walivyochunguza haya, hao Waislamu hata hivyo, waliwaita tu Mamajusi, nao wakaangalia hizo nyota. Waliwasha moto usiku, ulikuwa ni moto mtakatifu. Nao walimhudumia Mungu wao, kwa mioto hii mitakatifu, ulipowaka usiku. Basi wakakesha na kuomba. Na kila usiku walipanda hapa juu punde tu jua lilipotua, na wakayachunguza mambo haya. Kama tu ambavyo tunajumuika kwenye mikutano na kuchunguza Biblia, na Neno kwa Neno. Na walijua kila msogeo wa hizo nyota.

¹³⁵ Basi usiku mmoja walipokuwa huko juu, wakisoma. Na si ajabu lilikuwa jambo la kushtua sana wakati Mgeni alipoonekana miongoni mwao, Mgeni, hawakuwa wamewahi kuona Nyota hiyo hapo kabla. Hawakujua ni kitu gani kuhusu Hii, si ajabu walishtushwa. Ningewazia, usiku kucha waliangalia Hiyo. Hawakujua la kufanya kuhusu Hiyo. Jamani, Hiyo, Hiyo ilikuwa Ngeni. Katika mkusanyiko ule mkuu pale, walikuwa wameona Nyota ikining’inia papa hapa, kwamba Hiyo ilikuwa Ngeni, kitu kisicho cha kawaida. Hawakuwa wamewahi kuona kitu kama hicho. Kwa hiyo, upesi walianza kuchunguza kurudi katika Maandiko kuona kuwa hiki chote kinahusu nini. Bila shaka, wasingeweza kupata chochote katika maandishi yao wenyewe. Lakini walirudi kwa Danieli, wakaona, “Lipo Jiwe linakuja. Nyota ya Yakobo itainuka,” hata walijua kuna jambo lilikuwa likitendeka. Hapana shaka wote waliomba, na wakaenda kulala; wakijadili Hilo, pamoja. Na hapana shaka

walikuwa wameota usiku huo ya kwamba Mfalme wa wafalme alizaliwa duniani.

¹³⁶ Kwa kuwa, tunaambiwa katika kijipande cha gazeti la hivi majuzi, kuhusu Mamajusi kule, kwamba wakati nyota hizo tatu zilipopangana na kufanya nyota moja, kwamba Masihi alikuwa duniani wakati huo. Nao hakika walikuwa ni Mayahudi huko juu, wakisoma, kupata elimu yao katika unajimu. Kwa hiyo basi wakati wao—wakati walipoiona hiyo, walijua kwamba Yesu alizaliwa mahali fulani. Kwamba hawakujua mahali palipokuwa, lakini bila shaka walivuta nyasi kavu ili kutaka kujua la kufanya, jinsi tu, ni nani alikuwa aende huko. Kila mtu alitaka kuenda, kila mtu. Bali daima wao huchukua, kama nilivyosema muda mfupi uliopita, watatu ni ushahidi, kushuhudia, kurudi na kuwaambia kama ni kweli. Kwa hiyo walifanya nini? Walipakia mali zao, walipakia zawadi zao, na kila kitu, kumpelekea Yeye.

¹³⁷ Nashangaa tu usiku wa leo, ndugu, dada, kama sisi wakati mwingine, daima tunajaribu kuona ni kiasi gani tunachoweza kupata sisi wenyewe, wakati tunapaswa kuwa tukitoa kile tulicho nacho, kwa Kristo. Unaona, si kujifunza jinsi tunavyoweza kuwa werevu, na jinsi tunavyoweza kumshinda jamaa huyo mwingine, bali jinsi yote tuliyo nayo tunavyoweza kusalimisha Kwake.

¹³⁸ “Mungu nipe ndoto, hata nisingeamini hiyo,” niliwasikia watu wengine wakisema.

¹³⁹ “Siamini katika uponyaji wa Kiungu.” Nilikuwa nikimwonyesha jamaa fulani hivi majuzi kuhusu huo. Alisema, “Sijali ni madaktari wangapi wangetia sahihi majina yao, sijali ni mangapi unayosema, na ni nini kingekuwa, ama chochote zaidi,” kasema, “Siamini huo! Siamini huo!”

Nikasema, “Hakika huamini. Haukuwa kwa ajili yako.”

¹⁴⁰ Uponyaji wa Kiungu haukutumiwa wasioamini. Ulitumiwa waaminio. Kristo ni kwa ajili ya waaminio. Roho Mtakatifu ni kwao waaminio, pekee; si kwa wasioamini, haukukusudiwa wao. Ni jiwe la kikwazo lisilotambulikana kwao, daima litakuwa, daima lilikuwa hivyo. Si kwa ajili ya wasioamini. Ni kwa wale wanaoamini! Jambo ndilo hilo.

¹⁴¹ Sasa tunaona ya kwamba jamaa hawa, walikuwa ni waaminio, walitaka kujua. Walipakia kila kitu walichokuwa nacho, kuanza safari. Walitaka kujua kuwa hii ni nini, kweli. Sasa, walikuwa na safari ndefu, kwa hiyo wote waliweka mali yao pamoja, na—na kila kitu, kuwa tayari, pamoja na dhahabu, ubani, na manemane, na chochote kile walichokuwa nacho, ili kwenda kumwona huyu Mfalme. Walianza safari yao wakiwa na zawadi zao.

¹⁴² Pia, tazama, ili kumpata Mfalme huyu, waliongozwa na Ishara ya Kimbinguni, iliyotolewa na Mungu, sio na theolojia

ya mtu fulani. Walikuwa wameiona Hiyo katika Neno. Ilipaswa kuwepo pale, nao walifuata Ishara ya Kimbinguni.

¹⁴³ Laiti mtu angalikuwa tu na ujasiri waliokuwa nao! Laiti wangelikuwa tu na u—ufahamu waliokuwa nao! Mungu akitupatia kitu, kama ni Maandiko, shikilia Hilo!

¹⁴⁴ Mtu anasema, “Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Kuna ubatizo wa Roho Mtakatifu! Mko jinsi hasa Huo ulivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste, ndivyo Huo unavyokuja leo, uponyaji wa Kiungu, Nguvu za Mungu! Hakuna mtu awezaye kufa-...anayeweza kuifafanua katika Biblia, “Huo umeondolewa.” Ninaweza kukuonyesha ambapo Mungu amelipa Kanisa Huo! Utanionyesha Maandiko ambapo Yeye aliuondoa Huo? Hamna!

¹⁴⁵ Kwa kuwa, “Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Kwa kuwa ahadi ni...” Naye Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita wamjie.” Wote walioitwa! Roho Mtakatifu yeye yule, usiku wa leo, ni kama tu alivyokuwa wakati ule, kwa moyo mwaminifu. Kama sivyo... Je! ni jambo lisilo la kawaida sana kwako kumwamini Mungu?

¹⁴⁶ Kama vile Paulo alivyomwambia Agrippa, “Loo, Agrippa, hivi waweza, hivi waweza kukataa yale waliyosema manabii?”

¹⁴⁷ Hivi unaweza kukataa yale aliyosema Yesu, Mwenyewe, yale ambayo Biblia yenyewe hunena (ambayo ni Kristo, Neno lililopakwa mafuta)? Na kama Neno linakaa ndani yako, basi wewe ni mtu aliyetiwa upako na Neno. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, basi ombeni mtakalo, mtatendewa.” Huyu ni Kristo ndani yenu, akilitia upako Neno la wakati huu, wakati wowote walioishi. Mungu aliligawa Ne—Neno Lake kwa nyakati. Na kila wakati majira hayo yanapowadia, makanisa yote yamevurugika, ndipo Mungu anamtia mtu fulani upako, analituma duniani na kufanya Neno hilo litende hasa kama yeye alivyosema Hilo lilitenda. Hakika. Pia kuna Neno lililotabiriwa kwa ajili ya siku hii. Mungu anangojea kumpata mtu ambaye Hilo si la kigeni sana kwake, ili waweze kupakwa na Roho Mtakatifu, kuthibitisha kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, kuwa nuru inayoangaza, kuyapofusha macho ya asiyeamini. Nao watakufuru Hiyo, ingeleta haki juu yao; kwa kuwa amri ya Mungu ni ya haki, na hukumu inaweza tu kuja kwa haki Yake. Ndipo basi anaweza kuuhukumu ulimwengu, na kuutupa katika moto unaowaka, kama alivyofanya Wasodoma. Sasa angalia.

¹⁴⁸ Sasa tunaona, safarini, waliifuata Ishara waliyopewa na Mungu. Waliangalia. Hawakuchukua neno la mtu yeyote.

Hawakushuka kwenda kumtaka shauri askofu yeyote, au chochote kingine. Mungu aliwapa Ishara. Waliiona Hiyo *hapa*, Hiyo ilikuwa ni Kweli, nao wakafuata Hiyo. Iliongoza ile njia. Hiyo ilikuwa Ndiyo ambayo Maandiko yalibashiri. Walijua kwamba hii ilikuwa inakuja, nao wakaifuata. Nayo ilikuwa ni kitu gani? Ninaweza kuwaona wakiondoka, wakipunga mikono ya kwaheri, “Tutarudi siku moja, ndugu, tuwaletee ujumbe, kwa kuwa tunajua Hiyo ni kweli.” Nao wakaifuata Hiyo, chini kupitia milimani, chini kuvuka Mto Tigris, chini kupitia nchi tambarare, siku baada ya siku, miezi baada ya miezi, upesi walivyoweza kwenda, wakiiangalia ile Nyota.

¹⁴⁹ Wakati wa mchana, pengine, wangelala chini na kupumzika, na kulala, wageuke, wakasemezana, “Loo, hapana shaka ni ajabu tukifika kule; Mwanga huu wa Mbinguni, Nuru hii ya Mbinguni, Nuru hii tunayoiona, hii ya Kimbinguni!”

¹⁵⁰ Amina! Mnafikiri nimerukwa akili? Hapana. Angalia Mwanga huu wa Kimbinguni, Nuru hii tunayoitazama!

¹⁵¹ Sasa kumbukeni, hakuna mtu mwingine aliyeiona Hiyo, ilivuka kituo cha kuangalilia nyota baada ya kituo cha kuangalilia nyota, chini kwa Mamajusi baada ya Mamajusi. Lakini Hiyo ilitumwa kwa ajili yao. Ninaamini waliiona Hiyo, kwa sababu Biblia ilisema waliiona. Hakuna mwingine aliyeona Hiyo.

¹⁵² Hakuna mtu aliyeiona Nuru ambayo Paulo aliona, Kitu kile kile. Ilimwangusha chini, barabarani kuelekea Dameski. Lakini Hiyo alipewa Paulo.

¹⁵³ Hakuna mtu aliyemwona Roho Mtakatifu akija kama Nuru kutoka Mbinguni, Hua, ila Yohana. Yeye alimwona Huyo, alishuhudia. Alimwona Huyo, wengine wote hawakumwona. Yeye alimwona, kwa kuwa alikuwa akimtaazama Huyo.

Wale Mamajusi walikuwa wakitazama Hiyo!

¹⁵⁴ Na wakati unapomtaazama Huyo, wakati ukiwa tayari kuipokea Zawadi halisi ya Krismasi, Kipawa halisi cha Krismasi, Kristo-Kipawa cha Mungu, Roho Mtakatifu. Unamtaazama Yeye, utamwona. Ni Nuru ya Kimbinguni iliyotumwa duniani kutoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni, kumshuhudia Yesu Kristo.

¹⁵⁵ Sasa, hawakuchukua neno la mtu yeyote mwingine. Mchana, ilikuwa ni masumbuko. Walisema, “Loo, siwezi kabisa kungojea. Sijui ni umbali gani zaidi tutakaokwenda. Labda tutaenda hadi—hadi Yerusalemu, ama huko chini kwenye Nchi Takatifu, Palestina, maana huko ndiko unabii ulisema kwamba Huyu anapaswa kuzaliwa. Kwa hiyo tutaipata, siku moja.” Wakati wa usiku ukafika na giza likaanza kuingia.

¹⁵⁶ Kumbukeni, Nuru huangaza tu kwenye giza. Hiyo ndiyo njia ya pekee Hiyo inayotambulishwa. Kama tuliwahi kuishi

kwenye wakati wa giza, wakati wanadamu na kanuni za imani zimeondoa watu kutoka kwa Neno la Mungu, ni leo hii, wakati haya madhehebu yamewafungamanisha kwenye vitu vya kila namna isipokuwa Neno la Mungu. Kiasi kwamba, wangekuwa vipofu vya kutosha kuingia katika Baraza la Makanisa, mambo kama hayo, wakijiunganisha pamoja na kila namna ya wasioamini. Wakati, Biblia ilisema, “Wawili wanawezaje kutembea pamoja wasipokuwa wamepatana?” Na makanisa yetu yanaingia katika shirikisho kama hilo! Hakika, ni vipofu. Bali ni kwenye saa hiyo ya giza ambapo Nuru hutokea. Hapo ndipo Nuru huangaza.

¹⁵⁷ Basi wakitazama Hiyo. Ndipo usiku ulipowadia, wanashangilia na kusema, “Endelea tu kuongoza, kuongoza kuelekea magharibi, kuendelea bado, tuongoze hadi kwenye ile Nuru kamilifu.” Moja kwa moja, wakateremka na kuivuka mito, chini kupitia mafungu ya mchanga na kila mahali, walivyoenda, wakitaka tu kuipata Kweli yenyewe.

¹⁵⁸ Basi, tazama, Bethlehemu ilikuwa moja kwa moja kwenye mstari mmoja na Uyahudi kutoka mahali walipokuwa... Basi Yerusalemu ilikuwa moja kwa moja kwenye mstari wa Bethlehemu kutoka mahali walipokuwa wamesimama. Tazama. Loo, ni mfano jinsi gani, kama unaweza kuushika. Hii *hapa* Bethlehemu, na Yerusalemu iko *hapa* juu. Na kutoka mahali Mamajusi walikuwa wanakuja, ilibidi wafikie Yerusalemu kwanza, kabla ya kufikia Bethlehemu. Je! mnalipata? Hayo makao makuu ya kimadhehebu, makubwa mashuhuri, ya mtindo wa aina yake, (naam, bwana) Yerusalemu, ambapo madhehebu yote yalikutanika pamoja. Baraza kuu lilikutana huko, mwajua. Kwa hiyo wakati watu hawa, walipokuja, na wakaja kwenye mji huu, ndipo wakawaza, “Ile pale! Kama mtu yeyote atajua habari Zake, aweze kutuelezea Nuru hii kubwa ya ajabu, hao hapo makuhani wote wakuu. Hao hapo madaktari wa Uungu, hao hapo wa Ph.D., LL.D., na wote hawa hapa juu, watajua kila kitu kuhusu Hiyo. Loo, ndugu, Yerusalemu inaonekana! Haya twende, tutaipata.” Moja kwa moja wakaingia mitaani ghafla!

“Mnaenda wapi?”

“Tuna ujumbe mkuu.”

“Ni kitu gani?”

¹⁵⁹ “Yuko wapi Yeye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Hii Nuru ya ajabu hapa juu ni ya nini? Nani, yuko wapi Huyu?” Huku na huku mitaani, watu hawa matajiri, na ngamia waliopambwa vizuri, na dhahabu na uvumba, moja kwa moja kupitia kila barabara, kuteremka kupitia kila kichochoro, wakipiga mayowe, “Yuko wapi? Yuko wapi? Yuko wapi?” Lakini aligundua kwamba hawakuwa na jibu.

¹⁶⁰ Kilio kikubwa leo hii, “Ukomunisti uko juu yetu!” Loo, kila tangazo la redio, daima linashambulia Ukomunisti. Mnaweza

kuutambua Ukomunisti; bali ishara ya wakati, hamwezi kuitambua.

¹⁶¹ Yesu alisema, “Mnaweza kuutambua uso wa anga; bali ishara ya wakati, hamwezi kuitambua.”

¹⁶² Kila mara kuzungumza juu ya “Ukomunisti! Ukomunisti!” Heri mjue kwamba kuna jambo jingine linalofuatana nao.

¹⁶³ Tunaishi katika wakati gani? Ni nini ishara Mungu aliyosema Yeye angeonyesha mwisho, kabla haijatimia? Ni mambo gani aliyosema? Israeli katika mahali pake huko, mtini ukijirejesha tena. Angalia kila kitu kimekaa hasa mahali pake. Na kanisa katika hali ya Laodikia, Yesu akiwa nje, mkimbizi kwa kanisa Lake mwenyewe; kama tu vile Daudi alivyokuwa juu ya Bethlehemu, mkimbizi kutoka kwa watu wake wenyewe. Mkimbizi! Na Kristo, Biblia ilisema, katika siku za mwisho, alikuwa mkimbizi kwa watu Wake wenyewe. Hapo katika Ufunuo, mlango wa 3, katika wakati wa Laodikia tunaishi ndani yake, “Kristo yuko nje, akibisha, akijaribu kuingia ndani,” mkimbizi kwa watu Wake mwenyewe.

¹⁶⁴ Ilikuwa wakati huo ambapo wale askari wa vita walichukua panga, naye Daudi akalilia maji safi ya kunywa, nao wakapenya kupitia maili kumi na tano za watu, kumletea maji ya kunywa. Ndipo Daudi akayamwaga juu ya nchi, kama kafara, sadaka ya kinywaji.

¹⁶⁵ Naam, askari wa vita leo hii, Yesu anataka kinywaji kizuri, maji safi, ya pentekoste ya kale. Maji haya yaliyotuada, ya kimadhehebu yanamchefua. Litwae Neno la Mungu, na uvute Hilo, na upenye kupitia kanuni hizi zote za imani na kadhalika, mpaka tuweze kufikia mahali pale palipo na maji safi kwa ajili Yake; ibada halisi, ya kweli, moyo wa kweli, ambapo Yeye anaweza kumimina Yake, alifanye Neno Lake liishi katika siku hii. Atayapata. Alisema Yeye “Angerejesha Imani ya watu ielekee baba zao; Imani ya watoto.” Malaki 4 inatwambia itakuja, na itakuwepo. Msifadhaike, itakuwepo. Mungu amekwisha kusema hivyo, kwa hiyo hayo yatosha. Saa inasonga moja kwa moja. Naam, bwana. Bali leo hii tunaona kwamba zile ninii mashuhuri, leo ambapo tunaona . . .

¹⁶⁶ Ni kwa nini Ukomunisti unakuja? Ni kwa nini ulimwengu unamezwa? Ni kwa nini asilimia moja ya Urusi ingeweza? Hiyo tu ndiyo Ukomunisti. Asilimia tisini na tisa ingali Ukristo. Asilimia moja ya Urusi, inatawala ulimwengu wote, karibu, ulimwengu wa Mashariki. Ukomunisti. Kwa nini? Kwa nini ingeweza kufanya hivyo? Biblia ilisema ingefanya hivyo; Yeye analo jibu.

¹⁶⁷ Lakini unaona sasa tunajaribu kupiga vita *hiki* na *kile*. Na Kitu chenyewe ambacho Mungu alitutumia tukiangalie, hatuoni Hicho.

168 Walichukuliwa . . . mle ndani, wakijaribu kutafuta kujua ni vifungo vya aina gani wanapaswa kuvaa kwenye nguo zao, na kongamano lijalo, ni nani anayepaswa kuwa mnenaji wao mkuu, na kadhalika, kitu juu ya utaratibu wa hicho.

169 Na hapa walikuwa wale mamajusi wakitazama Nuru yao ya Kimbinguni, wakiteremka, kasema, “Nifikapo Yerusalemu, wataniambia ni nini Nuru hii ya ajabu, ya Kimbinguni iliyo juu yetu, inayotuongoza.” Na huku na huku mtaani wakaenda, “Yuko wapi? Amezaliwa wapi, Mfalme wa Wayahudi? Tuliona Nyota Yake Mashariki. Tumekuja kumsujudia. Tunayo dhahabu, uvumba, tuna kila kitu kwa ajili Yake. Yuko wapi? Yuko wapi?”

170 Wakasema, “Yuko wapi Nani? Kitu gani?” Hivyo ndivyo ilivyo leo hii. “Loo, hakuna kitu kama hicho kinachotendeka leo,” walisema.

“Loo, jua likitua, tunaona Nuru ya ajabu.”

“Kamwe sikuiona Hiyo.”

“Mwite mtu aliye kwenye mnara.”

“Je! uliona Nuru yoyote ya ajabu?”

“Ulisema nini?”

“Uliona ninii yoyote ya ajabu . . . ?”

171 “Hapana! Mna shida gani?” Mnaona, hawakuwa na jibu.

172 Hawanalo leo hii! Hawajui mambo haya ni nini, ambapo wanapaswa kuyajua, ambapo viongozi mashuhuri wa makanisa wanapaswa kuyajua mambo haya. Lakini Mungu daima hufanya kazi katika uchache, na unyenyekevu sana hata inapita juu yao, hawajui. Lakini hata hivyo Yeye hutimiza Neno Lake namna hiyo. Jambo ndilo hilo. Tunajisokota wenyewe katika mambo haya makubwa, na hatuwezi kusonga. (Mungu, tuweke huru na mambo haya, hata tuweze kuona ni wakati gani tunaishi.) Ikiwa Mungu anapaswa kufanya kazi kupitia ndoto tena, Yeye anaweza kukufunulia. Hakika, Yeye anaweza. Tunaishi katika siku za mwisho. Sasa sikilizeni. Loo!

173 Walikuwa hawana jibu la Nuru hiyo ya ajabu, hawakuwa nalo kwenye makao makuu. Wala hawanalo leo hii. Kwa hiyo walifanya nini? Waliitia Neno la Mungu. Hilo ndilo wazo. Walisema, “Hebu tuangalie kwenye Neno la Mungu, na tuone mahali mambo haya yalipo.” Basi walipoliitia Neno la Mungu, Mamajusi walikuwa werevu kuliko watu wengi leo hii. Mamajusi waliona, kulingana na Neno la Mungu, kwamba hawakuwa nalo, na hawakuwa wanaenda kulipata. Amina. Waligundua kwamba huo hata haukuwa ndio mji, hapo hata hapakuwa ndipo mahali. Alikuwa azaliwe katika Bethlehemu ya Yuda. Amina. Mdogo zaidi, aliye mnyenyekevu miongoni mwa hao wote, mahali padogo, duni, panyenyekevu, si pakubwa penye mtindo wa kipekee. Wenye hekima waliona upesi sana. Neno la Mungu lilifunua hiyo, kwamba hawakuwa nalo na walikuwa

hawaendi kulipata, kwa hiyo wakatoka katika mchafuko huo. Laiti tungaliweza tu kufanya vivyo hivyo! Wakionywa katika ndoto, walitoka katika mchafuko huo. Kwa hiyo, wakauacha. Haleluya, kwa ajili yao. Waliuacha.

¹⁷⁴ Baada ya kutoka kwenye mchafuko huo, ndipo cha Kimbinguni kikaonekana tena. Hicho hapo. Baada ya kujiweka huru kutoka kwenye mambo hayo. Baada ya wao kujiondoa kwenye lundo lote huko juu, kuzozana, kubishana, na kila kitu, huko chini kulikokuwa na makao makuu, na wote kuhani mkuu mashuhuri, na madaktari wa Uungu, wote wakitembea na Ph.D. yao, na kofia yao kubwa, nene ya kilemba, wasingaliweza kuona ile Nyota, kwa hiyo. Wakitembea hata... Mambo kama hayo huwapofusha watu wengi; majina makubwa, na watu wakubwa wakitembea huku na huku.

¹⁷⁵ Wengi wao walisema, “Vema, hakuna kitu kama hicho. Miaka mia nne, hatukusikia kitu kama hicho. Wana shida gani watu hao wendawazimu? Warudishe moja kwa moja huko India ambako ndiko kwao.”

¹⁷⁶ “Vema, kitu gani? Neno la Mungu, vipi kuhusu Hilo? Yeye alisema, ‘Ewe Bethlehemu ya Yuda, hu mdogo miongoni mwa majumbe wote wa Yuda? Bali kutoka kwako atakuja...’ Loo, tupo mahali pasipofaa,” walisema. “Hatutajiunga na wowote wa upuuzi huu.”

¹⁷⁷ Kwa hiyo, waligeuza ngamia wao na kuondoka. Mungu awabariki. Wakatoka hapo. Na punde tu walipoondoka, hapo ile Nuru ikatokea tena. Ya Kimbinguni ikaanza kufanya kazi ndani yao tena. Loo, jamani! Wakaanza kuifuata ya Kimbinguni hapo, Mamajusi wakatoka nje ya mfumo wao. Kwa hiyo baada ya wao kutoka katika huo, Nuru ya Kimbinguni kutoka Mbinguni ikawatokea tena.

¹⁷⁸ Mradi tu umefungamanishwa na kundi la wasioamini ambao hawaamini mambo haya, kamwe hutaweza, utakuwa kipofu kama popo. Jiweke huru na kila kitu; kama ni mama, baba, dada, kaka, dhehebu, ama chochote kile. “Yeye ambaye hatawaacha walio wake, na kunifuata Mimi, hata hastahili kuitwa Wangu. Yeye ashikaye plau, na kuanza, na hata akigeuka kuangalia nyuma, hastahili kulima kwa plau.” Ndugu, dada, hebu niwaambie, kuna Nuru halisi ya kweli ya Kikristo inayoangaza usiku wa leo, Hiyo ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo na hata milele. Jiweke huru na kila kitu! Na Yeye ni Neno. Yeye daima ni Neno. Neno la Mungu ni sahihi kikamilifu. Haifasiriwi apendavyo mtu fulani.

Unasema, “Linamaanisha *hili*.”

¹⁷⁹ Hilo linaamisha tu kile Hilo lisemacho. Biblia ilisema, “Halifasiriwi apendavyo mtu fulani.” Kama Hilo linasema, kama Hilo likisema, “nyeusi ni nyeusi, na nyeupe ni nyeupe,” hilo tu ndilo. Hilo ni Mkataa. Ndilo Yakini. Na kila mtu

aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu amefungamanishwa kwenye Hilo, haidhuru, hakuna kitu kitakachomtenganisha na Hilo. Amefungwa kwenye hilo Neno, kwa sababu ni Kristo. Kristo ni Neno. Na Kristo hawezi kusema uongo kuhusu Neno Lake, kwa kuwa Yeye ni Neno.

Ulisema, “Vema, ninajua Yeye alisema Hilo, lakini!”

¹⁸⁰ Hakuna “lakini” wala chochote kuhusu Hilo. Yeye alisema tu Hilo lilikuwa hivyo, na Hilo ndilo. Na Yeye hawezi kubadilisha Hilo. Hawezi. Yeye hawezi kubadilika. Alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe, hayatashindwa.” Litakuwa papo hapo katika majira Yake. Litaninii, kutakuwa na mtu pale atakayefanya Hilo kuangaza. Hiyo ni kweli.

¹⁸¹ Basi Mungu alinena hilo Neno, huyu Mwana angekuwapo, na Yeye alikuwa hapo, kufanya Hilo liangaze. Huyu hapo alikuwa Mgeni wa Kimbinguni; na wao walikuwa wakiangalia Hiyo, na wakaja moja kwa moja Kwake. Kwa hiyo waliacha kanuni ya kale ya imani, wakaanza kwa ya Kimbinguni tena, ndipo wakaondoka. Jinsi walivyoshangilia! “Wao,” Biblia ilisema, “walishangilia kwa furaha kuu hapo walipoiona Nuru hiyo ikija tena.”

¹⁸² Loo, ndugu, dada, jinsi ingekuwa vizuri kama kila mmoja wenu, kama kila mmoja wetu, sisi, mimi, kama kila mmoja wetu angeweka kando haya yote hapa mapambo ya Krismasi, unaona, tuachane na huku kote kubadilishana zawadi, mmoja na mwingine, upuuzi huu wote wa ulimwenguni; na kuondoa tu majivuno yetu na kuyaweka chini, na kukanyaga kitu hicho chini ya mguu, tuseme, “Bwana Yesu, niongoze hadi kwenye ile Nuru kamilifu.” Angalia jambo fulani la Kimbinguni likitendeka. Roho Mtakatifu atakuja kwa njia ya ajabu. Mnaona?

¹⁸³ Moja kwa moja waliondoka, wakifuata ya Kimbinguni. Basi waliacha kitu gani? Waliifuata Ishara ya Kimbinguni ya siku hiyo, sasa kumbukeni, Ishara ya Kimbinguni, iliyotolewa na Mungu. Je! nyinyi nyote mnaamini kwamba hiyo ni kweli? Hiyo ilikuwa ni Ishara ya Kimbinguni, iliyotolewa na Mungu. Waliifuata Ishara hiyo mpaka wapakata Neno lililofanyika mwili. Je! mnaamini Yeye alikuwa lile Neno lililofanyika mwili? Ishara ya Kimbinguni, iliyoahidiwa kwa ajili ya siku hiyo, iliwaongoza hadi kwenye Neno lililofanyika mwili.

¹⁸⁴ Ndugu, dada, Yeye atafanya vivyo hivyo usiku wa leo. Ishara hii kuu kutoka Mbinguni, tuliyo nayo, Roho Mtakatifu akiishi miongoni mwetu, ifuateni Hiyo. Kitu fulani kinasogea ndani ya moyo wako, “Ninajua ninapaswa kupokea Huyu. Ninajua ninapaswa kufanya zaidi ya kujiunga na kanisa.”

¹⁸⁵ “Nina biashara nzuri, ni—ninajua inanawiri.” Ndugu, je! unajua moja ya siku hizi mshtuko wa moyo huenda

ukakuchukua saa kumi asubuhi, na inakubidi kuiacha hiyo biashara? Basi unaenda wapi baada ya hapo?

¹⁸⁶ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ikithibitishwa katika mwili wako mwenyewe, wewe ndiwe yule mtu aliyezaliwa na Roho Mtakatifu. Si ungependa kuwa na hiyo? Hiyo si ingekuwa ndiyo zawadi kubwa kuliko zote za Krismasi ambazo mtu yeyote angeweza kupata? Kipawa cha Uzima wa Milele. “Mungu aliupenda sana ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asiangamie, bali awe na Uzima wa milele.”

¹⁸⁷ “Tumeona Nyota Yake Mashariki na tumekuja kumsujudia.”

¹⁸⁸ Ustaarabu umesafiri pamoja na jua, kutoka Mashariki, kuja magharibi. Tuko kwenye Pwani ya Magharibi sasa, Mashariki na Magharibi zimekutana, hatuwezi kusonga mbele zaidi. Ustaarabu ulio wa kale zaidi ni China, moja kwa moja nyuma upande ule mwingine wa dunia. Kumbuka, imeenda . . .

¹⁸⁹ Pia dhambi imesafiri pamoja na ustaarabu. Na sisi . . . Ninajua ni vigumu kusema hili. Lakini, ndugu, dada, hata mawazo na makusudi ya moyo wa mwanadamu, mtu aliyepakwa na Roho anaweza kusimama, na wewe umeiangalia na kuiona kwa wengine. Unasimama na kumwangelia mtu, waache tu waseme neno moja au mawili, anaweza kuona papo hapo hao wadudu wakiruka; unaona, wao—wao wanashika upako pamoja nao. Kila wazo la binadamu daima ni ovu. Ni kama tu ilivyokuwa katika siku za Nuhu, mpaka hata ilimhuzunisha Mungu kwamba Yeye alimwumba binadamu, Yeye akasema, “Nitamwangamiza binadamu kutoka kwa uso wa dunia.” Na tumerudi kwenye wakati huo hata hivyo, tena. Angalia.

¹⁹⁰ Bali Yeye analo Kanisa dogo analotaka kuchukua. Anao maelfu mengi wamelala, wamelala katika ardhi; zamu ya kwanza, zamu ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano, ya sita. Na hii ni zamu ya saba. Kumbukeni, hapo ni wakati Yeye anapokuja, katika zamu ya saba. Na kwenye zamu hiyo, aliwakuta bikira werevu, na mabikira waliokuwa wameishiwa na Mafuta katika taa yao. Mafuta ni mfano wa Roho Mtakatifu. Ikiwa hujapata Hayo katika taa yako usiku wa leo, ndugu yangu, dada, mbona msichukue Hiyo, Zawadi kubwa zaidi ya Mungu ya Krismasi.

¹⁹¹ Mnajua, leo hii tunapata zawadi kubwa, nene, tunaifunga, na kuchukua dola tatu kuifunga, na kuweka kila namna ya mapambo juu yake. Na mara nyingi unafikiri ni zawadi kubwa. Basi mwanamke mmoja akisimama kwenye duka hivi majuzi, wawili wao, wakizungumza, mmoja alisema alikuwa anaenda kumnunulia baba yake . . . Kasema, “Nini,” akiongea na dada yake, kasema, “Unaenda kumnunulia baba nini?”

¹⁹² Kasema, “Ninaenda kumnunulia jozi ya karata, na—na katoni ya sigara.”

¹⁹³ Akasema, “Nimemnunulia kisaga cha wiski, na,” kasema, “Ninaenda kuifunga.” Mnaona, mapambo ya nje siyo, hayatangazi kilicho ndani. Mnaona?

¹⁹⁴ Lakini Mungu anayo Zawadi ya Krismasi kwa ajili yako usiku wa leo. Aliifunga katika hori. Nje haikuvutia sana, lakini, loo, Ndani ni Uzima wa Milele. Hivi hutaliacha tukio hili la Roho Mtakatifu kuyapiga maisha yako usiku wa leo, na kukuongoza kwenye Nuru ya Milele?

Hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja.

¹⁹⁵ Katika utulivu wa wakati huu, maskini ninii hii iliyokatikakatika, kama ningeuia ujumbe wa Krismasi, moja ya hizo. Ikiwa kweli unauamini kuwa ni Kweli, nawe hujawahi bado kupata Nuru hiyo ya Milele, hujamruhusu Roho Mtakatifu mkuu akuongoze kwenye hiyo Nuru, waweza kuzungumza sasa hivi moyoni mwako, na kusema, “Bwana Yesu, ninataka kuipata hiyo Nuru. Sijali yale mtu yeyote mwingine asemayo, ni mimi, mimi ndimi, ninataka kuipata hiyo Nuru.” Je! mnaweza kuinua mikono yenu sasa, huku mmeinamisha vichwa vyenu? Inua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham, kwa kweli ninataka kuipata hiyo Nuru.” Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki. Na Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mwingine, inua mkono wako, useme, “Ninataka, ninataka kufanya hivyo, ninataka Zawadi ya Mungu ya Krismasi.” Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, mama. Mwingine, sema, “Ninataka Zawadi ya Mungu ya Krismasi. Nitumie Hiyo, Bwana, sijali ni kitu gani Hiyo. Kama Hiyo ikija katika hori, kama Hiyo ikija katika zizi, sijali jinsi Hiyo inavyoonekana ya kufedhehesha kwa ulimwengu, jinsi inavyonibidi kuonekana mwenye aibu kwa ulimwengu.” Unajua, vipawa vikuu vya Mungu daima humfanya mwanadamu kujiadhibisha visivyo kawaida.

¹⁹⁶ Mwangalie Musa, mwanatheolojia mashuhuri, msomi mashuhuri, bali siku moja alikutana na Nuru upande wa nyuma ya jangwa. Alivua viatu vyake. Mtu mwenye umri wa miaka themanini, na masharafa yakining’inia chini kufikia kiunoni mwake, akaweka mke wake na mtoto mchanga juu ya nyumbu, na kuenda huko chini Misri. Ambapo alikuwa na jeshi zima kumfanyia mapinduzi siku moja, naye alishindwa; sasa anarudi akiwa tu na fimbo iliyopinda, akienda Misri, kuliteka taifa hilo. Kwa nini? Alikuwa ameipata ile Nuru, ile ya Kimbinguni.

¹⁹⁷ Basi Kitu hicho kidogo kinachonyonganyonga moyoni mwako usiku wa leo, hicho ni cha Kimbinguni, hicho ndicho Nuru ya wakati. Hivi hutaiacha Hiyo ikuongoze kwa Yesu Kristo, Ambayo inaweza tu kukupa Uzima? Je! yupo mmoja ambaye hawajainua mikono yao, angeweza kusema, “Nikumbuke, Ndugu Branham, katika maombi sasa”? Mungu akubariki. Mwingine? Akubariki. Mwingine, mtu mmoja?

Mungu akubariki. Mungu akubariki, kijana mwanamume. Mwingine? Mungu akubariki, ewe kijana. Je! atakuwepo mwingine?

¹⁹⁸ Sema, “Ninataka kufuata, ninataka kuifuata Nyota ya Asubuhi, Kristo. Ninataka kufuata na kumpata Yesu wangu leo hii. Ninataka kuondokea haya yote hapa mapambo ya Krismasi na kadhalika, kwa sababu siku moja yatateketezwa na moto usiozimika.” Na wale wote wanaochukuliana nayo, watateketezwa pamoja nayo. Ulimwengu, mwenye dhambi, ataadhibiwa, wataangamia pamoja na ulimwengu. Watu wapendao ulimwengu wataangamia pamoja na ulimwengu. Na kama unayo, japo, bado kuupenda ulimwengu kumo ndani yako, na unataka kujitoa kabisa kwa Yesu Kristo na Neno Lake usiku wa leo, inua mkono wako. Tena sasa, mtu yeyote ambaye hajainua. Mungu akubariki. Akubariki. Ninasema tu hilo. Mungu akubariki, mama.

¹⁹⁹ Hujui, dakika moja huenda mtu akainua mkono wao. Unasema, “Hiyo inaleta tofauti gani, Ndugu Branham?” Tofauti kati ya mauti na Uzima.

²⁰⁰ Kama mkono huo uliinuliwa namna *hiyo*, na kwa kweli ulimaanisha hilo, kuna Kitu fulani karibu nawe. Ni nini Hicho? Hicho ni ile Nuru ninayozungumzia. Hicho ni ile Nuru inayokwambia. “Nimekuwa makosani. Upo ulimwengu ndani yangu. Siutaki tena. Nitainua mikono yangu.” Huo ni ushuhuda.

²⁰¹ Kumbukeni kile, je! mnajua mkono ulioinuliwa ni nini? Katika kila lugha chini ya Mbingu, mkono ulioinuliwa ni kujisalimisha, ishara ya kujisalimisha. Unapoinua mikono yako, jeshi lolote, popote unapoinua mkono wako, ni—ni ishara ya kimataifa ya kusalimu amri.

²⁰² Ni wangapi usiku wa leo, moja kwa moja kwenye nukuu hii sasa, utainua mkono wako, useme, “Ninasalimisha yote, Bwana. Ninajisalimisha. Ni—nimemaliza. Ninajisalimisha.” Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hiyo ni kweli. Hilo ni jema. Loo, jamani.

²⁰³ Sijui kama mpiga piano pale angeweza kwenda kwenye piano wakati tukiomba.

²⁰⁴ Baba wa Mbinguni, ninatambua Hiyo ilisema, “Wote walioamini walibatizwa.” Hayo ndiyo yote yanayohitajika, Bwana. Ikiwa wanakuamini Wewe, jambo fulani halina budi kutukia. Hao ni Wako, ni nyara za ibada hii ndogo ya Neno la Mungu; Uwepo wa Yesu Kristo hapa kwenye kundi hili zuri la watu usiku wa leo, waliokusanyika hapa, dhifa hii ndogo. Bali usiku wa leo tunajua kwamba Wewe upo hapa. Kwa namna fulani, labda, huenda hatujaiona Hiyo kwa macho yetu, lakini tulihihi Hiyo kwa hisi yetu nyingine, hisi yetu ya ndani, hisi ya kuona ndani ya moyo wetu, dhamira yetu. Nafsi yetu ilitunenea, na kusema, “Tuko katika Uwepo wa Yesu Kristo: Zawadi kubwa

kuliko zote za Krismasi, Zawadi ya kwanza halisi ya Krismasi kwa mwanadamu kutoka kwa Mungu.”

205 Na, hata hivyo, kati ya zawadi zote tulizopokea, wengi wetu hawajapokea ile Zawadi kubwa bado. Tunaomba, Mungu, kwa ajili yao usiku wa leo wanapoinua mikono yao, wanataka hii inayojitosheleza. Wameegemea upande huo, Baba. Jalia . . .

206 Marabi walifanya hivyo, pia, wengi wa waalimu mashuhuri wa siku ile waliegemea upande Huo, ila waliogopa kujitokeza na kujitoa kikamilifu mara moja, na kuamini Hiyo; na kuukubali Ujumbe, na Nuru ya wakati, Neno lililothibitishwa. Kulikuwa na wengi waliofanya hivyo.

207 Bwana, wapo wengi hapa usiku wa leo, ishirini au thelathini katika kundi hili dogo la watu. Kama nimekadiria idadi ya chini, au zaidi, nisamehe. Bali, Bwana Mungu, labda wengi hivyo, takriban, wameinua mikono yao. Wako tayari kujisalimisha. Mungu, wape Yesu, wape Roho Mtakatifu maishani mwao. Jalia huu uwe ndio wakati mkuu zaidi maishani mwao. Jalia waende nyumbani usiku wa leo, kama Yusufu, wakitafakari mambo haya moyoni mwao, “Ni kwa nini nilinua mkono wangu? Ni nini kilichonisababisha kufanya hivyo? Ilikuwa hata nikafanya hivyo? Hata hivyo, nimedai kuwa Mkristo kwa miaka, bali Kitu fulani kilinambia kuinua mkono wangu.” Washiriki wa kanisa, hata wahudumu, waliinua mikono yao, Bwana. Ninaomba ya kwamba Wewe utawajalia baraka hii. Tujalie hayo.

208 Tena naomba Malaika wa Bwana aje, na kusema, “Msiogope, hii ndiyo Nuru ya siku hii. Hii ndiyo Nuru ya wakati. Nuru za jioni zinaangaza.” Nabii alisema, “Itakuwa Nuru wakati wa jioni, kabla tu ya machweo ya jua.” Pia, Bwana, tunaona machweo ya jua la wakati, hivi punde itaingiliana na Umilele. Tujalie, Bwana, kwamba kila mmoja wao atampata Yesu usiku wa leo. Kwa kuwa niliomba hayo katika Jina Lake. Amina.

209 Hebu tuinua tu mikono yetu katika hali ya kujisalimisha, namna *hii*, tunaposimama kwa miguu yetu.

210 Ninaenda kuwaomba jambo fulani. Nyinyi mlioinua mikono yenu muda mfupi uliopita, ni—niliwaombea. Hayo tu ndiyo nijuayo kufanya, ni kuomba. Ninaenda kuamini kwa ajili yenu. Ninaamini kwamba yale niliyoomba, Yeye ananipa, kwa sababu Yeye aliahidi kuwa angefanya hivyo. Hawezi kusema uongo. Hawezi kusema uongo. Jambo la pekee—jambo linalozuia hilo kutendeka ni ninii yangu . . . lingekuwa ni kutokuamini kwangu. Ninaamini kwa ajili yenu, kwamba kwa kweli mlimaanisha hayo. Naye Mungu anaenda kuwapa Roho Mtakatifu. Anaenda kuwapa Huyo, maana mliomba mpewe Huyo, mnataka kujisalimisha.

211 Na kama mlifanya hivyo, ninawaambieni kile ninachotaka mfanye. Ninataka utafute kanisa fulani zuri linaloamini ubatizo wa Roho Mtakatifu, nenda huko. Nenda huko. Na

ikiwa uko kwenye kanisa kama hilo, mwendee mchungaji wako, umwambie, sema, “Niliinua mikono yangu hivi majuzi usiku, kwenye mkutano mdogo.” Hata haikulazimu kumwambia ulikuwa wapi. Sema, “Niliinua mikono yangu, ninataka uombe pamoja nami, mchungaji. Ni—ni—ninatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninamtaka Huyo. Sina budi kuwa Naye. Sina budi kuwa Naye, ili kuishi. Ni lazima tu niwe na Huyo! Nimeona Nuru.” Loo, Mungu akupe Huyo. Je! mtafanya hivyo sasa?

²¹² Na sasa vile kila mtu humu ndani, tunapoenda kuimba, “Natoa, natoa yote. Yote kwa Kristo, Mwokozi wangu, natoa yote.” Vema, hebu tuinue mikono yetu sasa, na kufumba macho yetu, tunapoimba.

Natoa yote,
Natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

Natoa yote,
Natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

²¹³ Je! mnamaanisha hivyo? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sasa ninawatakeni mfanye jambo fulani kwa utamu sana sasa. Mtu fulani aliyesimama karibu nawe, washike mkono, na useme, “Ndugu, nilimaanisha hilo. Niombee.” Hebu tufanye hivyo, sote pamoja, tulifanye hivi sasa.

[Ndugu Branham anazungumza na wale walioko kwenye jukwaa—Mh.] Ndugu, nilimaanisha hilo. Niombee. Mungu akubariki. Mungu abariki . . . mimi.

Hilo ni jema. Hilo ni sawa. Loo, hivi haliwafanyi kujisikia vizuri? Nilimaanisha hilo.

²¹⁴ Sasa ikiwa kwa kweli kutoka moyoni mwetu, tunamaanisha hilo, tunasalimisha kila kitu, mapenzi yetu wenyewe, njia zetu wenyewe, kila kitu tulicho nacho, tunasalimisha kwa Kristo, hebu tuinue mikono yetu tena na kuimba.

Natoa yote,
Natoa yote,
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Natoa yote.

²¹⁵ Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa, na tuimbe. [Ndugu Branham anaanza kuvumisha, *Natoa Yote*—Mh.] Sasa iweke tu nia yako Kwake. “Na. . .” Ninawatakieni Krismasi njema zaidi, kwamba Mungu ataituma Nyota Yake kutoka Mashariki, iliyochomoza Mashariki, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, nayo itawaongoza kwenye Neno lililofanyika mwili. [Ndugu Branham anaendelea kuvumisha, *Natoa Yote*.]

Natoa yote,
Natoa (mikono juu kwa Mungu),
Yote Kwako, Mwokozi wangu mbarikiwa,
Na . . .

Mungu akubariki, Tony.



TUMEIONA NYOTA YAKE NA TUMEKUJA KUMSUJUDIA SWA63-1216

(We Have Seen His Star And Have Come To Worship Him)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marriion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumatatu jioni, tarehe 16 Desemba, 1963, kwa ajili ya dhifa ya Kimataifa ya Ushirika wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, katika Hoteli ya Ramada kule Tucson, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org